# *ULIMWENGU UNAPOROMOKA*

Bila shaka ni baraka kubwa kuwapo hapa, kusikiliza shuhuda hizi nzuri kutoka kwa ndugu hawa wanaompenda Bwana wetu Yesu. Sasa, ningali ninaishi kwenye—kwenye. . . Niseme nini basi? Kichocheo nilichopata kutokana na huo ujumbe, mmoja wa hizo, jana jioni; bila shaka, zote. Lakini umenichechemua moyo, kwa huyu ndugu hapa, nikifikiria juu ya kujaribiwa kwake; kama Yeye alivyomfanyia, alivyomjaribu Ayubu, na, lakini alikuwa maradufu mwishoni. Na ninafikiri ni baraka sana kuketi hapa, kusikiliza ushuhuda wa mtu fulani, ndipo unaweza kulinganisha maisha yao.

2 Nilihubiri juu ya jambo hilo hivi karibuni huko Phoenix, "sisi kujitambulisha na Kristo," na kujitambulisha pamoja Naye katika Biblia. Kama tungaliishi katika siku ile, tungejitambulisha na kundi gani?

3 Basi, jana usiku, wakati Ndugu Crow, ninaamini hilo lilikuwa ndilo jina lake, yule ambaye alituletea ujumbe huu mzuri sana wa ushuhuda wake. Tulikuwa kule tumeketi, muda mfupi uliopita, tukilinganisha maisha yetu sisi kwa sisi. Na sote wawili tukiwa ni Wabaptisti; wanandondi wa kawaida, na kadhalika, na mapigano yetu ya mwisho, kile kilichotukia. Na tena basi kwa kweli niliufurahia. Nilifurahi kwamba waliurekodi.

4 Na sasa, asubuhi ya leo, ninajua tuna dhi—dhifa ama chakula cha mchana hapa, kwa ajili ya wahudumu, sasa hivi tu. Na—na. . .[Ndugu fulani anasema, "Hapana. ni wanaume wote, asubuhi ya leo."—Mh.] Ati nini? ["Wote—wanaume wote."] Wanaume wote. Ndiyo. Halafu basi, usiku wa leo, nafikiri kwamba hiyo dhifa iko kwa. . .["Wahudumu, mtu ye yote anayetaka, wanaume wote wanaotaka kuja."] Naam. Mwanamume ye yote, mhudumu, ama mtu wa kawaida. [Ndugu Demos Shakarian anasema, "Dhi—dhi—dhifa bado ni mpaka saa sita na nusu."] Saa sita na nusu. ["Kwa hiyo hizo ni saa mbi—mbili, saa mbili na nusu, saa mbili tangu sasa. Unaona?"] Mtu mkarimu sana, Ndugu Shakarian, na mke wake.

5 Dada Williams, nilitaka kusema jambo fulani, lakini sitalisema. Ndugu Carl, ushuhuda wake, muda mfupi uliopita, ulikuwa ni mzuri sana. Kwa hiyo mimi. . .Mara ya kwanza niliyopata kujua jambo hilo, kadiri nilivyokujua, lakini ulikuwa—ulikuwa ni mzuri sana. Ni—ninajifunza somo kwa mambo haya yote. Sivyo? Sawa.

6 Kwa hiyo, basi, usiku wa leo, ninazungumza juu ya somo, usiku wa leo, Bwana akipenda, "Hapo wao wakamsulibisha Yeye."

7 Na sasa, leo, kwa ajili tu ya kubadilisha msimamo wangu, kabla hatujazungumza juu ya somo fupi. Niliingia katika jiji lenu, jana, kwa mara yangu ya kwanza, itakuwa ni mara yangu ya pili kuzungumza. Nilikuwa na ninii. . .Huko New Mexico, nilikuwa na mkutano wakati fulani huko Carlsbad, kwa masiku machache. Lakini kamwe sijapata kuwa na majaliwa ya kufika hapa mahali hapa pazuri hivi, hapo nyuma. Nami—napenda kufika mapema, na kwa namna fulani nizoee mambo yalivyo mahali hapo na kuona ninii. . .mji huo unahitaji nini. Sasa, hatupaswi kabisa kufika kwenye mji, kama wahudumu. . .

8 Sasa, wafanyabiashara, huu ni mkutano wa Injili. Mko hapa kuzungumzia juu ya biashara zenu, na shida zenu na baraka, kuzishiriki mkiwa pamoja. Na hilo ni jambo zuri sana.

9 Lakini kama mhudumu wa Kristo, tunakuja hapa kupata kujua hali ya kiroho. Halafu si kuja hapa kusikiwa wala kuonekana, bali ni kuja hapa kufanya jambo fulani la kumtukuza Mungu, kulileta jambo kwenye—kwenye ufahamu mzuri zaidi wa Mungu. Na mara moja nilibadilisha somo langu, asubuhi ya leo.

10 Na sasa, kabla ya kusoma Maandiko, nafikiri kama tunaweza kusimama kwa kusudi la kubadilisha namna ya kukaa kwa muda mfupi sana, kwa maombi mafupi. Na sasa, kabla hatujaomba, kama kuna mtu ye yote hapa ambaye angependa kukumbukwa katika maombi haya, tafadhali inua tu mikono yako. Haidhuru iwe ni kitu gani, Yeye anajua kilicho chini ya mkono wako. Na yangu yote miwili imeinuliwa.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tunapomkaribia Yeye.

11 Baba yetu wa Mbinguni, sisi ni watu tuliopendelewa sana kuketi pamoja leo katika Ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, kwa Roho mmoja, sote tumebatizwa katika huu Mwili mmoja, na tuna majaliwa ya kuketi hapa pamoja na kushiriki baraka za shuhuda za hawa, watoto Wako.

12 Na sasa, kwa kuwa muda umeenda sana, tusingependa kuingia wakati huu ulio muhimu sana, kwa nafasi yangu ya kuzungumza na watu, kwa wasiwasi, ama nikifikiria inabidi tuharakishe kutoka. Lakini tunaomba ya kwamba utatuliza mioyo yetu, kwa kitambo kidogo, na tuendelee kusikiliza zaidi mausia Yako kwetu, na maonyo Yako. Nami nitakungojea, Baba, kwa ajili ya mambo haya.

13 Na sasa tunaomba ya kwamba utabariki tawi hili la wafanyabiashara, hawa Wakristo, wanaume wa full Gospel, ili kwamba ushuhuda wao uenee kila mahali, kwa utukufu na heshima ya Bwana wetu.

14 Na sasa tunafuraha kujua ya kwamba wakati unakuja ambapo falme za ulimwengu huu zitakuwa falme za Bwana wetu na za Kristo Wake, hivi kwamba tutatawala na kumiliki

duniani pamoja Naye, miaka elfu moja. Tunautarajia wakati huo. Na kusikia hawa watu wakizungumza juu ya majaribu yao, na jinsi Shetani alivyomchukua Bwana wetu mpaka juu ya kilele cha mlima, na katika dakika moja akamwonyesha serikali zote na falme za dunia, na akamuuzia, bali Yeye alizikataa kata kata, kwa sababu alijua ya kwamba siku moja atakuwa mrithi kwazo. Nasi hatuangalii mambo yale yanayoendelea kwa kitambo sasa, bali tunaangalia mwisho wa mambo, ambako zawadi zinatolewa.

15 Baba, tunaomba, asubuhi ya leo, ya kwamba utaifanya mioyo yetu iwe na kicho mbele Zako, tunaposikiliza. Ninaomba ya kwamba Wewe utanena nasi, Bwana, kupitia midomo ya binadamu. Jalia tukusikie kwa masikio ya kibinadamu. Na kisha tujalie, kwa upande wetu, tutii kila kitu ambacho unatuagiza. Tunakungojea sasa wakati tunapolisoma Neno Lako lililo takatifu sana, ambapo msingi we—wetu wa imani unakaa katika Neno lililoandikwa. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mnaweza kuketi.

16 Na sasa, katika Neno, ningewatakeni mfungue kwa ajili ya kusoma Maandiko machache, hasa sana katika sehemu mbili, kwa ajili ya mihitasari michache ambayo nimeiandika hapa, ambayo ningetaka kuninii, kama somo la shule ya Jumapili, kutoa mawazo kwa dakika chache, kama mtaniwia radhi. Kumbukumbu la Torati 4, kwanza, Kumbukumbu la Torati 4:10 na 11. Ningetaka kusoma vifungu hivi.

> *Siku ile uliyosimama mbele za Bwana wako huko Horebu, Bwana aliponiambia, Nikusanyieni watu hawa, nami nitawasikizisha maneno yangu, ili wajifunze kunicha mimi siku zote watakazoishi duniani, wakapate na kuwafundisha watoto wao.*
>
> *Akakaribia, mkasimama chini ya ule mlima; mlima ukawaka moto mpaka katikati ya mbinguni, kwa giza na mawingu, na giza kuu.*

17 Na tena katika Wabrania 12:25. Tunasoma maneno haya kutoka Waebrania 12:25.

> *Angalieni msimkatae yeye anenaye. Maana ikiwa hawakuokoka wale waliomkataa yeye aliyewaonya juu ya nchi, zaidi sana hatutaokoka tukijiepusha . . . tukijiepusha na yeye atuonyaye kutoka . . . yeye atuonyaye kutoka mbinguni:*

18 Sasa, haya kwa namna fulani ni Maneno yasiyo ya kawaida kusomwa kwenye—kwenye kiamshakinywa cha wafanyabiashara, bali Bwana na ayabariki mioyoni mwetu. Na sasa ningetaka kuchukua somo hili dogo. Ambalo nilikuwa . . . Asubuhi ya leo, lililokuwa moyoni mwangu kuzungumza juu ya somo, “Damu kwenye Ujumbe.” Nami nililikwepa tu hilo,

kwa sababu fulani, bila kujua ni kwa nini. Lakini ninataka kuchukua somo hapa, asubuhi ya leo, la kipekee, bali niliite: *Ulimwengu Unaporomoka*. Hilo ni somo la kigeni, bali ni—ninajisikia nikiongozwa kuzungumza juu yake: *Ulimwengu Unaporomoka*.

19 Sasa tuko kwenye jambo hili, ikiwa tunayoita "Ijumaa kuu," ama Ijumaa kuu ya Mungu. Sijui ni kwa nini tunaiita hivyo, "Ijumaa kuu." Lakini tuko mwanzoni tu, kwenye mlolongo mwingine wa—wa sikukuu, siku takatifu ambazo ulimwengu hutenga, ulimwengu wa Kikristo, ku—kusherehekea katika kukumbuka, matukio makuu ya Maandiko yaliyotukia katika siku zilizopita, mambo makuu yaliyotukia. Nasi tunazitumia na kufanya ni wakati wa kusherehekea mambo hayo yaliyotukia. Kama Mungu...Kama—kama Mungu angalikuwapo hapa katika ulimwengu huu wa Kikristo wakati huu, na kile tunachoita ulimwengu wa Kikristo, sijui msimamo Wake ungekuwaje kuhusu mtindo wetu wa kusherehekea tulio nao kwa—kwa ukumbusho wa sikukuu hizi na nyakati ambazo—ambazo zimekuwako.

20 Na watu wanakusanyika pamoja, katika matumaini ya kupata kitu fulani. Wanataka kujua, kupata jawabu ama namna fulani ya mfumo fulani, wakati wa tegemeo kuu, kuudumisha ulimwengu wetu pamoja. Tunakusanyika hapa asubuhi ya leo kwa kusudi hilo.

21 Watu hukutanika katika jamii mbalimbali, kutaka kujua kama kuna shida yo yote. Sote tunajua ipo. Na kuna shida ulimwenguni, nasi hatuna budi kujitahidi kutaka kujua jambo hili. Na watu wanakutana katika jamii hizi ili wapate ufumbuzi wa mambo. Hili limetukia mara nyingi katika ulimwengu wetu, kile tunachoita "kuporomoka." Tunaishi katika wakati ambapo ninii ye—yetu...si taifa letu pekee, bali ulimwengu wetu wote unaporomoka. Inaonekana kana kwamba hakuna kitu kilicho na msingi, hivyo ni kusema, kinachoweza kusimama.

22 Tulijaribu katika mambo mengi sana mbalimbali. Tume—tumejaribu kuuelimisha ulimwengu, kufikia kwenye maelewano. Tu-...Na tumekuwa na mifumo mbalimbali ya Shirikisho la Mataifa, na Umoja wa Mataifa, na kadhalika, kujaribu kuleta maelewano kwa mwanadamu. Ulimwengu wa Kikirsto umejaribu kuwaelimisha watu wapate kuelewana. Tumejitahidi kuwaingiza kwenye madhehebu wapate kuelewana. Na inaonekana kana kwamba tumerudi nyuma moja kwa moja, kama ilivyotukia daima, mifumo yote inaporomoka, kuna kasoro fulani.

23 Tunataka, kulifikiria jambo hili kwa uzito, kwa dakika chache zinazofuata. Hebu tu usiingilie jambo hili sasa, ati useme tu, "Vema, tulienda kule tu na kuketi kitako. Tulipata

kifunguakinywa. Tukasikia shuhuda, na kadhalika.” Lakini hebu, kwa mioyo yetu yote, tuliingilie jambo hili na kulitafakari.

24 Kumbukeni, ni uhai wetu, na hakuna jambo lililo muhimu zaidi ya uhai wetu. Hakuna jambo lililo muhimu zaidi, haidhuru tunapata faida gani ulimwenguni, ama jinsi gani tunakuwa tu wakubwa hapa, lakini hatuna budi kufikia kikomo cha safari. Na halafu ninii . . . Huo ni wakati muhimu sana, na inatupasa kuuendea kwa unyofu wote tuujuao.

25 Wakati, watu katika zamani nyingine, wakati watu walipojaribu kupata njia za kujihami, nao wakaunda mifumo. Na jinsi pekee wanavyoweza kwenda kwenye mfumo mwingine wo wote, mbali na ile Mungu aliyoiweka, ni kuondoka kwenye Neno Lake. Watu katika nyakati zile nyingine wamefanya jambo hili, nyakati zilizopita. Wote walijaribu kuondoka, na wakajaribu kuutawala ulimwengu, na kufanya mfumo wa siasa, na mambo mbali mbali kujaribu kutawala na kuushikilia u—ulimwengu pamoja. Na, wao, kusudi wafanye jambo hilo, hawana budi kuondoka kwenye mpango wa Mungu wa kufanya jambo hilo. Unaona? Wao wananinii . . . Mungu ana njia ya kuweka jambo hili pamoja. Na njia pekee ambayo watu wanaweza kushika njia nyingine, inambidi kuondoka kwenye njia ya asili.

26 Unaona, kabla hapajakuwapo na uongo, hapana budi kuwapo na kweli ambayo huo uongo unatokea huko, kwa sababu uongo ni ukweli uliopotoshwa. Dhambi zote ni—ni haki iliyopotoshwa. Hivyo yote ni dhambi ilivyo, ni kuninii . . . Unaona? Ibilisi hawezi kuumba cho chote. Yeye hupotosha kile Mungu alichoumba. Kuna Muumba mmoja tu, na huyo ni Mungu. Uongo ni ukweli uliopotoshwa. Uzinzi ni tendo sahihi lililopotoshwa. Na jambo lo lote ni, ambalo ni baya, ni haki iliyopotoshwa.

27 Kwa hiyo, basi, kuchukua mfumo mwingine wo wote wa kuudumisha ulimwengu pamoja, mbali na mfumo wa Mungu, ni upotovu. Kwa hiyo cho chote kilichopotoshwa hakina budi kuwa na mwisho, kwa sababu kila kitu kilichokuwa na mwanzo kina mwisho. Ni mambo yale yasiyokuwa na mwanzo, ambayo hayafi hata, hayana mwisho kamwe.

28 Na kuna kitu kimoja tu ambacho hakikuanza kamwe, na hicho kilikuwa ni Mungu. Kwa hiyo, njia pekee tunayoweza kuishi Milele ni kuwa na Uzima wa Mungu Mwenyewe ndani yetu, na huo ni Uzima wa Milele. Nasi . . . Mungu alijigawa Mwenyewe miongoni mwetu, na akatoa Roho Yake kama alivyofanya Pentekoste, na alionekana katika mifano ya Moto, kutoka katika ile Nguzo ya Moto iliyojigawa Yenyewe miongoni mwa watu, apate kutoa Uhai Wake Mwenywe kwa watu. Na kupitia katika jambo hili, nia ya Kristo inapaswa kuwa ikitenda kazi miongoni mwetu.

29 Na Mungu ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Na lingali ni Mungu, hiyo ni kweli, ni Neno. Na tunapoliacha Neno, basi tumemwacha Mungu. Yesu alisema, "Mkikaa ndani Yangu..." Fumbo lao ndilo hilo. Siri ndiyo hiyo. "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo." Unaona? Wazo ndilo la kwanza. Neno la Mungu linapaswa kuishi *hapa*.

30 Huwezi kuchukua kanuni za imani na itikadi, na kadhalika, na kuzishindilia ndani yako, na kuchukua mafundisho fulani ya sharti na kuyachanganya na Neno la Mungu, kisha umfanye Mungu akubalie jambo hilo. Inapaswa kuwa ni Neno la Mungu kweli kweli, lililo safi, lisiloghoshiwa, na ni hivyo tu. Ni hivyo tu. Mungu hatachanganyikana na kitu cho chote kilichopotoshwa. Yeye ni Mungu kweli kweli, kote kote.

31 Sasa, daima, katika nyakati zote, tumekuwa na mambo haya, ya watu ambao—ambao walijaribu kupotosha Neno la Mungu, na kuchukua mifumo ya namna nyingine. Na—nao wanaona, baada ya muda mrefu, wanaona kama tu tunavyoona siku hizi, mwaka huu wa 1963, wanaona ulimwengu ukiporomoka. Hakika unaporomoka. Kwa maana, hauwezi kushikamana, si zaidi ya vile Danieli alivyosema katika—katika ono lake, ile fasiri ya wale wafalme, ya kwamba, si zaidi ya vile chuma na udongo vitachanganyika pamoja, wala Neno la Mungu halichanganyikani na kitu kingine cho chote. Halitachanganyikana tu. Halina budi kuwa ni Neno. Hivyo tu.

32 Sasa tunaona ya kwamba siasa, katika siku za—za ulimwengo alioishi Nuhu, zilikuwa zimetawala. Na mpango wa elimu na ulimwengu ulioshamiri kibiashara wa siku hizo ulikuwa—ulikuwa umejirembesha sana hata kufikia mahali ambapo ku—kujengwa kwa mjengo, ya mapiramidi na masifinksi, na kitu ambacho hatungeweza kujenga kwa vyo vyote vile.

33 Kama mtu ye yote alipata kuwako huko Misri, na kuona ya—yale mapiramidi na kadhalika, hatuna kitu cho chote siku hizi ambacho kingeweza kujenga moja kama hilo. La. Lakini walikuwa wameendelea mbele zaidi kuliko sisi, katika elimu. Walikuwa wameendelea mbele zaidi katika sayansi.

34 Ndipo wamekuja kutambua, ulimwengu umeanza kuporomoka. Naye Mungu akawapelekea ujumbe, bali waliukataa. Na ulikuwa ni ujumbe rahisi, rahisi sana, kupitia kwa mkulima wa kawaida sana, bali wao waliukataa na kuupuuza. Ndipo ulimwengu wao ukaporomoka. Naam.

35 Jambo lilo hilo lilitukia Sodoma, wakati wa Sodoma, wakati uzinzi ulipokuwa u—umepamba moto. Nao walijenga miji, na kadhalika. Lakini, wakaja kutambua, Mungu alituma mfumo

wake kule, ndipo wao wakaukataa, ndipo ikaporomoka. Daima itaporomoka.

36 Sasa, jambo lile lile lipo leo. Tuko katika siku kama ile ile iliyokuwako kule. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu," kitu hicho chote kikivunjika na kuporomoka. Ninii . . . Kimejengwa juu ya mchanga, nacho hakina budi kuchukuliwa na maji. Na tunaona wakati huo mkuu kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo i—ilivyo leo.

37 Na katika wakati wa kuja kwa Bwana wetu Yesu, katika siku za mwanzoni za—za wakati alipozaliwa, tunauona ulimwengu ule, katika siku ile, ukiporomoka, wakati alipozaliwa ulimwenguni. Tunaona ya kwamba ule ulimwengu wa kidini . . . Kama ambavyo ninataka kuzungumzia habari zake, usiku wa leo, juu ya kule kusulibishwa, kuhusu kitu kama hicho. Wao . . . Tunaona ya kwamba Wayahudi walikuwa ndio kwanza wauchafue mfumo huo ambao Mungu alikuwa amewapa, katika Neno Lake, mpaka hakukuwa na uaminifu tena, dhabihu za—za—zao, ingawa walitoa dhabihu, kimaandiko. Nao wakatoa dhabihu zao. Wakati Wayahudi . . .

38 Hakuna kitu kilicho kitamu sana kuliko Mungu kutakabali kibadala. Wakati, mwanadamu alipokuwa amefanya dhambi, na Mungu akaridhia kibadala. Akiwa amejaa neema, alikukuwa amejaa neema, kufanya jambo kama hilo. Wakati Myahudi aliposhuka akaja, akiwa na fahali wake ama mwana-kondoo wake, apate kwenda akamtoe kama dhabihu, naye alilifanya jambo hilo kutoka ndani ya moyo wake kabisa, lilikuwa ni jambo kuu. Lakini, baada ya kitambo kidogo, likawa ni jambo la desturi katika familia. Walishuka tu wakaenda wakatoa dhabihu ya fahali, na, "Vema, wakati wa kutoa dhabihu umewadia, kwa hiyo tutaenda tu na kumtoa sadaka fahali huyu."

39 Ikawa ni de—desturi. Karibu nimeshawishika kuamini ya kwamba hivyo ndivyo ilivyotukia kwa mfumo wetu wa Kikristo. Kwamba, katika madhehebu yetu mbalimbali na—na jamii zinazojiita Wakristo, tumefikia mahali hapo. Ambapo . . . Na hata kwetu sisi, Wapentekoste. Sasa, kumbukeni, dawa ni ya familia nzima. Na sisi, Wapentekoste, tunajiingiza katika jambo hilo. Nasi tumeshangaa.

40 Ulimwengu wote wa Kipentekoste leo unaporomoka. Mfumo wote, wa Wamethodisti, Wabaptisti, Mpresbiteri, m—mfumo wote wa kidini unaporomoka. Tunaona jambo hilo. Tunajua hiyo ni kweli. Ulimwengu wote wa siasa zetu za kitaifa unaporomoka. Jambo zima limefikia mwisho wake. Kama Isaya alivyosema, "I—imejaa vidonda vitokavyo usaha." Ni, ninii tu, mwili wote umeoza.

41 Kuna jambo fulani halina budi kutukia. Nalo litapita mfumo ama ufahamu wo wote ulioundwa na mwanadamu, ambalo itabidi kurudisha kitu hicho chote kwenye hali zake asilia tena.

42 Ninajua hii ni picha mbaya sana, bali ni kweli. Inatubidi tuangalie jinsi mambo yalivyo hasa, wala hakuna haja ya kurudia kunukuu jambo lo lote, au kulifunika, hasa, bali ni kutoka na kusema ukweli kulihusu. Kweli ni kweli, na kosa ni kosa. Unaona? Na ni lazima tuangalie jambo hilo.

43 Basi tunaona mataifa siku hizi. Maisha ye—yetu ya siasa na ya taifa yameoza kabisa. Yote yamejaa—yamejaa mambo, ama upotovu wa televisheni, kila aina ya mizaha michafu, kinyaa, na vichekesho, tena mbele ya vijana wetu.

44 Na shu—shule zimeoza kabisa! Jamani! Mimi natokea Arizona. Ni—nilikuwa kwenye moja ya shule kubwa, majuzi, nikawaona hao wasichana na wanaume, vijana, huko kwenye kampasi, wakigaragaza kule. Nikasema, "Natumaini haitanilazimu kumpeleka mmoja wa watoto wangu katika mahali kama hapo."

45 Na penye ufisadi kama huo, hata hivyo, panaitwa—panaitwa Marekani. Baadhi ya mambo mabaya sana niliyowahi kuona ni tabia za Wamarekani katika—katika sehemu mbali mbali za humu nchini. Kila mara tunazungumza juu ya nchi nyingine. Ingekuwa ni busara kufagia milangoni petu kabla hatujaweza kusema jambo lo lote kuhusu mtu mwingine.

46 Na sisi Wapentekoste tunapaswa kufagia milangoni petu kidogo, pia, kabla hatujaanza kupigia makelele mambo ya Kipresbiteri na Kibaptisti. Kwa sababu, mfumo wetu umeoza vivyo hivyo na unaporomoka kama yao inavyoporomoka. Unaona? Tunaishi tu katika siku hiyo.

47 Na sasa tunataka kukumbuka jambo hilo, katika siku hizi ambazo Yesu alizaliwa, tunaona ya kwamba walikuwa na mfumo wa aina hiyo. Hawakuwa na uaminifu. Walienda huko tu na—na eti mtu amekuwa ni Myahudi, na ametahiriwa siku ya nane. Naye kwa kweli amekuwa ni Myahudi.

48 Vema, tuna jambo lile lile leo. Wanawachukua kuwapeleka kanisani na kuwafanya watoto kuwa Wakristo. Na—na halafu jambo la kwanza, unajua, mbona, wao ni wafuasi wa kanisa hilo. Na unawauliza kama wao ni Wakristo. "Hakika, mimi ni Mkristo. Mimi ni Mmarekani."

Na wakati mmoja kwenye mstari wa maombi, nilimwuliza bibi mmoja, wakati mmoja, "Je! wewe ni Mkristo?"

49 Akasema, "Vema, ningetaka kukufahamisha, mimi huwasha mshumaa kila usiku." Sasa, kana kwamba jambo hilo lilikuwa na uhusiano wo wote na Ukristo.

50 Mmoja alisema, “Mimi, vema, mimi ni—mimi ni fulani. Mimi ni mfuasi wa Kipresbiteri. Mimi ni *hili*.” Hilo bado halina maana yo yote.

51 Hilo si zaidi ya vile unavyoweza kumchapa ng’ombe alama. Ungeweza—ungeweza kuweka chapa ya Hereford juu ya ndege mla mizoga. Haitaleta tofauti yo yote. Hilo halibadilishi upande wa ndani wa mtu. Wewe uko vile ulivyo, kwa kuzaliwa kwako, na hiyo ni katika Kristo. Unaona? Tu—tuna alama hizi tu, na—na kadhalika. Ni, sisi . . . Tumeingiza jambo hilo lote katika mfumo fulani na katika mchafuko.

52 Na tunaona jambo hilo hivyo katika wakati wa kuja kwa Bwana Yesu. Kama nilivyofikiria, kuleta maisha Yake, kwa kuzaliwa Kwake na huduma Yake; halafu, usiku wa leo, kusulibishwa Kwake. Jambo hilo lote linaanza kuoza. Walilitangua Neno la Mungu, kwa mapokeo yao, kwa hiyo ulimwengu wote ulikuwa ukiporomoka. Kila taifa lilikuwa likitarajia mtu fulani ama mfumo fulani ambao ungeweza kuwatoa kwenye jambo hilo, hiyo ni kusema, kuwashikamanisha. Walikuwa wamepotoka sana hata walijua wasingeweza kustahimili kwa jinsi waliyokuwa wakiendea, na—nao walikuwa wakitafuta kitu fulani cha kuwashikamanisha.

53 Kama hiyo si picha ya ulimwengu wetu siku hizi, mimi sijui ulimwengu. Ndiyo. Ndiyo picha ya ulimwengu wetu siku hizi. Kila kitu kinatafuta mfumo fulani ama—ama kitu cha kutushikamanisha pamoja. Ndiyo picha ya siku hizi. Ulikuwa ukitafuta mfumo fulani au kitu fulani ambacho kingeuzuia usiporomoke. Kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo na sasa, tena. Imejirudia tena.

54 Ulimwengu wa kidini wakati huo ulikuwa ukimtarajia Masihi aliyeahidiwa. Wayahudi wote wangekwambia, waamini imara sana, “Hakika, tumekuwa, miaka elfu nne, tukimtarajia Masihi. Nasi tunaamini ya kwamba Yeye—Yeye anakuja. Hakika, tunaamini jambo hilo.” Ulimwengu wa siasa wa siku ile ulikuwa ukimtarajia Masihi. Na mataifa mengine yote, kila moja, lilikuwa likimtarajia Masihi. Na wakati alipokuja, walimfanyia tu kama walivyofanya katika nyakati nyingine.

55 Walikuwa wakitafuta kitu cha kuwafanya kitu kimoja katika siku za Nuhu. Na wakati Mungu alipowatumia mjumbe, nini kilitukia? Wakaukataa.

56 Na wao wanautafuta, nyakati zote. Hivyo ndivyo inavyotukia. Wao wananinii tu . . . Mungu atawapelekea huo. Na ndipo wananinii tu . . . Wanaupuuza. Kwa sababu, kwa nini? Hautoshelezi ladha yao. Unaona? Wao—wao hawautaki jinsi vile Mungu anavyotaka kuutuma. Wanautaka jinsi wao wanavyoutaka. Walikwisha uwazia, jinsi unavyopaswa kuwa, na usipokuja namna hiyo, basi, “Si wa Mungu.” Unaona? Hivyo ndivyo imekuwa daima.

57 Ni jambo lile lile leo. Hauji katika ladha ya ladha yetu ya kitheolojia. Bali unakuja kwa nguvu za thibitisho la dhihirisho la ahadi ya Mungu kwa ajili ya wakati huo. Hakika. Bali, hata hivyo, kama ilivyokuwa wakati huo, wao waliukataa. Waliukataa wakati huo. Wameukataa siku hii, kwa maana hautimizi matarajio yao ya siku hizi kulingana na vile watu wanavyoutarajia.

58 Mungu ana tarajio. Mungu anajua yatakayotukia, kwa maana yeye hana kikomo, kwa hiyo hakuna shida yo yote. Kila kitu kinaendelea vizuri kabisa, kwa maana Yeye hana kikomo. Naye anaweza kutabiri mwisho tokea mwanzo, kwa maana Yeye ni Mungu. Usifikiri Shetani anamfunika kwa cho chote. Loo, la. Loo, la. Yote yanatukia yapate kuonyesha sifa Zake, hivyo tu. Mungu mkuu asiye na kikomo angewezaje, ambaye alijua kila kitu, na kuacha kila kitu . . . Ni sifa za Mungu tu zikionyeshwa.

Na wewe unaonyesha maisha yako, kwa upande mmoja ama mwingine.

59 Na hiyo ndiyo sababu mifumo yetu inaingia, nayo inaweza kukubali cho chote kile, ni njia ya mfumo, ni kwa sababu tu kwamba wao wanaiacha njia ya asili iliyoumbwa ambayo Mungu aliwatengenezea kulifanya jambo hilo. Njia—njia yake ya kutuma vitu mara nyingi hairidhishi ladha yetu. Sijui, siku hii, kama Mungu angalijibu kilio chetu kwa ajili ya Masihi wetu tunayemlilia sana siku hii, sijui kama tungefanya jambo lile lile walilofanya huko nyuma.

60 Sasa, sote tunatazamia jambo fulani. Tunajua hivyo, daima. Kila mtu anatazamia jambo fulani. Nilikuwa nikisikiliza, umati huu. Ninawasikiliza wafanyabiashara. Ninaenda kwa wahudumu. Ninaenda kwa madhehebu mbalimbali. Kila mtu anatarajia jambo fulani. Taifa hili, ukisikiliza mazungumzo ya siasa, wanatarajia jambo fulani kutokea. Ni kitu gani? Ninalisikia katika wafanyi biashara Wakristo. Ninalisikia kwenye mikutano. "Loo, ule wakati mkuu unaokuja! Ule wakati mkuu unaokuja!" Sasa, ninyi kumbukeni tu, utakuja kwa njia tofauti kabisa na ile mnayodhania itakuja. Unaona? Haitakuwa hivyo hata kidogo, yale unayofikiria. Haijakuwa hivyo kamwe. Unaona?

61 Na ulimwengu wetu wa siasa, leo, na ulimwengu wetu wa dini, ni kama vile ulivyokuwa kabisa katika siku za kule kuja kwa kwanza kwa Masihi. Umechafuka. Mfumo wote umeoza. Siasa zetu, zisingeweza kuwa mbaya zaidi ya hapo. Na dini yetu, sioni jinsi ingaliweza kuwa mbaya zaidi kuliko ilivyo sasa. Kitu hicho chote kimepotoka; ulimwengu wetu wa siasa, mifumo ya kujitengenezea, na—na mitindo. Tuna ninii tu . . .

62 Tunataka kila kitu ninii tu, kila kitu, ili tusipate shida, na kupumzika tusifanye kazi, na kustarehe. Maisha hayakukusudiwa kuwa rahisi. Maisha ni mapambano. Kitu cho

chote chenye uhai kinafanya kazi kwa bidii. Angalia miti, jinsi inavyokazana. Angalia kila kitu chenye uhai; ni mapambano. Na wakati tunapojaribu kuchukua namna fulani ya mfumo wa kuchukulia mambo kwa urahisi, basi tumekosea. Nasi tunajua kuna kasoro.

63 Nilisikiliza, leo, te—televisheni yetu na—na vipindi, na magazeti yetu, na mambo haya yote yanayoendelea, na kila mtu anafanya mzaha. Kujaribu kupata . . . Marekani imejengwa juu ya wingi wa vichekesho, namna fulani ya mzaha, kama vile Ernie Ford na hao nyota wote wa televisheni. Kufanya ninii yote . . . Na sinema zetu zimepotoka sana, hazingeweza tu kupotoka zaidi ya zilivyo. Hivyo tu.

64 Inanikumbusha juu ya mvulana mdogo aliyekuwa akipita makaburini, akipiga mbinja, akijaribu kujifanya afikiri haogopi. Bali hiyo ndiyo sababu yeye anapiga mbinja. Unaona? Anaogopa. Na hiyo ndiyo shida. Mnajaribu, ulimwengu leo, unajaribu kulicheka. Marekani ni mzaha na tunajua namba yetu imeitwa. Imepimwa kwenye mizani na kuonekana kwamba imepungukiwa. Kama Mwenyezi Mungu hatararua taifa hili vipande-vipande, Yeye atakuwa—Yeye atawajibika kwa Sodoma na Gomora, kuifufua na kuomba msamaha kwa kuichoma moto. Kweli. Tumeangamia. Ulimwengu mzima umekwisha. Unaporomoka, wala hakuna njia ya kuuokoa. Umetenda dhambi ukamaliza siku zake za neema.

65 Ati tunazungumza juu ya uamsho? Tunaishi kwenye majivu ya ufufuo. Umepita, muda mrefu uliopita. Na hata hivyo tunajaribu kujenga mfumo fulani juu ya kitu fulani. Loo, jamani! Imeoza. Hatuna budi tena kuanza kuninii . . . Wao, vipindi vyetu vya dini, hakika vimekuwa uvundo katika mianzi ya pua ya Mungu, kama ilivyokuwa katika siku za Israeli, mpango wetu wa Kimethodisti, mipango yetu ya Kibaptisti, mipango yetu ya Kipentekoste.

66 Mtu fulani aliniambia, muda mrefu, si muda mrefu uliopita, "Uliwalaumu hao Wapentekoste sana, mbona unaambatana nao?" Ninawapenda. Hiyo ndiyo sababu yake. Upendo husahihisha. Kama hausahihishi . . .

67 Vipi kama kadogoo angesimama hapa barabarani, na—na yuko huko nje akitengeneza lundo la matope katikati ya barabara, mahali ambapo hayo magari yanapita? Nawe useme, "Kadogoo, nakutakia la heri, kipenzi. Haikupasi kuketi huko nje. Utakapokuwa tayari, ingia ndani." Huo si upendo. Humpendi mtoto wako. Nawe ungemtoa kutoka hapo, na kumtupa nje ya barabara hiyo. Kisha uchukue fimbo na kumfundisha hapaswi kwenda huko nje tena, endapo kweli unampenda.

68 Na hiyo ndiyo shida ya huduma yetu siku hizi. Wako huko. Ni njia ya kujipatia riziki. Ni jambo la kimadhehebu, nao

wanaogopa kupeleka Injili jinsi ipaswavyo. Mpaka wafikie hapo, inakupasa kuileta kwenye ile kweli. Kuna kasoro fulani, nasi tunajua jambo hilo. Tunang'ng'ania mifumo badala ya Ufalme wa Mungu. Nasi tunajua kuna kasoro fulani. Imeoza.

69 Nafikiri siku zetu za Kipentekoste zimekuwa ni uvundo. Tunapiga muziki, na kuruka-ruka kwenye—kwenye marefu ya kanisa, na kucheza, na kukimbia-kimbia huku na huko. Na wanawake wamekata nywele, na rangi ya midomo kwenye nyuso zao, na vitu kama hivyo. Na kukimbia huku na huko pale, wanacheza katika Roho, pamoja na . . . wanavyoiita, wakiwa wamevaa rinda, iliyobana sana hata ngozi yenyewe ya mwili ingeweza kutokeza nje. Na ati na tunamtarajia Mungu kukutana nasi katika mfumo kama huo? Kamwe hatafanya jambo hilo. Unajua, Mungu hafuati masharti yako. Unafuata masharti Yake la sivyo usije kabisa.

70 Loo, tunazungumza juu ya watu kuingia na kumpokea Roho Mtakatifu, na mambo kama hayo. Nami nimeninii . . . Bila shaka, ninafurahia jambo hilo. Ninalifurahia. Bali angalia hapa yale tuliyofanya, enyi marafiki. Tumejenga madhehebu yetu juu ya ishara fulani, kama vile tunavyochukua kunena kwa lugha. Ninaamini katika kunena kwa lugha, hakika, bali kila kitu kinachonena kwa lugha hakina Roho Mtakatifu. Mimi ni mmishenari. Nimeona wachawi wakinena kwa lugha na kufasiri, na kutoa tafsiri ya kweli ya lugha hiyo, na kunywa damu kutoka katika fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kumwita Ibilisi. Kweli. Rudini kwenye Neno la Mungu ambako ndiko kwenu. Yakimbieni mambo haya. Maisha ndiyo yanayonena ndani ya binadamu, Maisha ya Kristo. Unawezaje uwe wa Kristo na ushikilie taratibu hizi? Basi angalia mahali tulipofikia?

71 Kanisa la Pentekoste, wakati lilipoanza, miaka hamsini iliyopita, na Roho Mtakatifu akaanza kushuka na watu wakapokea karama ya kunena kwa lugha, ndipo mkaanza kuingiza kila kitu ndani yake, mkifanya *hiki* madhehebu, na *kile*, na kile *kingine*. Basi angalieni mahali mlipo leo, mpaka kitu hicho chote kimeoza. Hiyo ni kweli. Mfumo wote umepotoka, na unaporomoka tu pamoja na ulimwengu wote. Kila kitu hakina budi kufanya hivyo.

"Bali tumepokea Ufalme usioweza kutikiswa."

72 Sasa, kumbukeni, siasa zetu zimeuendea ulimwengu. Makanisa yetu yameuendea ulimwengu. Yote yamechafuliwa, siku zetu, leo.

73 Wakati, tulizoea kuwa, zamani, wakati ninapoweza tu kukumbuka, wakati kanisa letu la zamani la Kibatisti chini kule katika jimbo la Kentucky, wakati walipokuwa na hao wanawake wa mtindo wa kizamani na wanaume wameketi kule, pamoja na hao. Mhubiri, jana usiku, Ndugu Crow, akizungumza juu ya mabibi hao waliovaa kofia. Na—na walikuwa na mazoea

ya, wanachoita, kutakaswa. Ama, basi wangetoka huko nje na kupaza sauti, na—na pini za nywele zingeanguka kutoka kwenye nywele zao wakati walipolia, na—na kuenda huku na huku kwenye marefu ya kanisa, wakimsifu Mungu. Mbona, ndugu, watu hao walikuwa na dini ya kutosha kukifanya kizazi hiki cha Kipentekoste kujionea aibu. Na, tena, hakika. Hao walikuwa ni Wabaptisti, Wamethodisti, na Wapresbiteri. Hakika.

74 Halafu mnawaita Wakentucky kundi la—la wajinga. Hebu acha Mkentucky fulani, mama wa mtindo wa kale, aone binti yake akitokea mtaani, ndani kule milimani, awe amevaa kaptura, kama vile ilivyo kwenu ninyi na bibi zenu na ninyi wengine mnazovaa. Hebu na aingie, asubuhi, akiwa nusu uchi, amejinyonganyonga, na rangi zake za makucha, rangi za midomo, ama cho chote kile, usoni mwake mwote, amekuwa huko nje na maskini ricky fulani usiku kucha, kwenye gari la anasa, akizurura, aingie. Angemcharaza, kwa moja ya hizo fimbo za mwerezi, asingeweza kutoka kitandani kwa muda wa miezi sita.

75 Halafu ati unajiita Mpentekoste? Angalia siku tunayoishi. Na wahubiri wanaogopa sana kusema neno kuhusu jambo hilo mimbarani, wanaogopa watafukuzwa kwenye shirika lao. Kweli. Kweli. Tunahitaji kitu fulani cha "kurudi kwenye Neno la Mungu." Si kurudi kwenye msisimko fulani, si kwenye *maongezi* fulani juu ya "kurudi kwenye Neno," bali ninamaanisha moyo na nafsi, ndani ya mtu binafsi, kurudi kwenye Neno la Mungu. Hakika. Ulifanyaje? Kwa nini wanaogopa kusema jambo hilo? Ukianza kuongelea habari zake, madhehebu yako yatakutupa nje. Hiyo ni kweli.

76 Hivi karibuni nilisoma hadithi fupi ambayo mtu fulani alinipa, hapa gazetini. Ni, inatoka huko Memphis, Tennessee. Inaitwa, *Hadithi ya Tony Fontane*. Kama unataka kuona tangazo la kuchekesha, soma hiyo gazetini, linadaiwa kuwa ni la Kipentekoste. Linadhaminiwa na Assemblies of God, moja ya mashirika makubwa sana ya Kipentekoste. Liangalieni. Nitaliacha hapa, mwanamke aliyekata nywele zake anayefanana na Yezebeli na mwanamume mmoja Mfaransa pale. Mnaita huko ni kuongoka? Mbona, ni mhemko. Hakuna kitu kwake kinachoelekea kwenye wokovu. Ro-Roho wa Mungu atamsafisha mwanamume ama mwanamke, na kuwafanya tofauti na vile walivyokuwa. Ni kweli. Lakini tuna kitu gani? Tuna Hollywood, iliyoingizwa kwenye Upentekoste. Ni kitu gani? Kwa sababu ya programu zao za elimu, na jambo hilo.

77 Hiyo ndiyo sababu hatuwezi kuwa na ufufuo. Hiyo ndiyo sababu jambo fulani haliwezi kuendelea. Hiyo ndiyo sababu tumekuwa tukiendelea, kwa maana mtu huna kurudi kwenye Neno tena, ndugu yangu. Hakika.

78 Ni jambo la kusikitisha sana, kwa ufadhili wa shirika la Kipentekoste. Usingeweza kusema Mungu alidhamini kitu kama hicho. La hasha. Lakini ni kitu gani? Ni kitu kilicho na mvuto. Mmeangalia televisheni mno kupita kiasi. Mmefanana sana na ulimwengu. Hiyo ndiyo sababu kitu hicho chote kimeoza, na kupotoka, na kinaporomoka. Hakika. Kinanuka, mbele za Mungu.

79 Sijali unazungumza kwa lugha jinsi gani, jinsi gani unavyopiga makelele na kukimbia huku na huko chumbani. Sijali unafanya *hivi* kiasi gani, ama unakua mkubwa jinsi gani, kwamba mnao waheshimiwa wangapi miongoni mwenu. Hilo halina uhusiano wo wote nalo. Mnapaswa kutupilia mbali baadhi ya hao, na kumleta Roho Mtakatifu miongoni mwenu, ambaye atawasafisha, na kufanya kanisa halisi kutokana na ninyi. Hivyo ndivyo ilivyo. Hiyo ni Kweli kabisa. Tu-. . .

80 Tunachohitaji, leo, ni nabii wa Bwana ajitokeze jukwaani, akiwa na Neno la Mungu, ambaye hatapatana na mambo ya ulimwengu. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hilo ndilo tumaini pekee lililopo kwa—kwa ma—maisha yajayo, mtu fulani atakayeshika Injili; si kwa kuvaa glavu za raba za kikasisi, kuamini kiasi *fulani* na kuondoa kiasi *fulani*. Loo!

81 Na tofauti zetu za kimadhehebu sasa zimetuingiza kwenye karibu madhehebu mia tisa mbali mbali. Mashemasi wetu wanakubaliwa kuoa wanawake wawili ama watatu, na bado wanatumika kama mashemasi. Mara kwa mara mhubiri ataliacha kanisa moja na aende kwenye lingine, kwa sababu kuna pesa zaidi mahali fulani kuliko mahali pengine. Kundi kubwa zaidi mahali fulani na kanisa bora zaidi, na kadhalika, apate vipenzi na vibaraka. Na, loo, jamani!

82 Tunataka watu walioitwa na Mungu, wakali, kutokea kule nyikani, wakiwa na ujumbe kama wa Yohana Mbatizaji, ambao utawachuna ngozi baadhi ya hawa wanaojiita mashirika ya kidini.

83 Ni dhambi. Ina—inamhuzunisha Roho Mtakatifu. Mara nyingi, katika maono ambayo Bwana anatoa . . . Vema, sitaingilia jambo hilo sasa. Unaona? Niliulizwa hivi majuzi . . . La, nitaninii tu . . . Ninapenda ninii . . . Samahani.

84 Sasa, kuhusu Ujumbe wa "kuporomoka." Mambo yale yanayoendelea, mambo yale ambayo hayapaswi—hayapaswi kuwa mageni kwa kanisa, hata hivyo ni mageni. Hebu wazungumzie hayo, hawataki kuamini. Nuhu aliponena, hawakuamini. Musa aliponena, hawakuamini. Manabii waliponena, hawakuamini. Hakika. Walikuwa tayari wameunda mifumo yao. Ndiyo, bwana.

85 Ule uadilifu mzuri, loo, jamani, wa—wa umama wetu, ule uadilifu wa wanawake wetu Wapentekoste, umesujudu

kwenye madhabahu ya yule mungu mke, Hollywood. Na kile tulichokuwa tukiita "uadilifu," tunakiita "mtindo." Ni aibu.

86 Mtu fulani aliniambia, si muda mrefu uliopita, alisema, "Ndugu Branham, hivi huwezi kuwaacha hao wanawake, kukata nywele zao, na kuvaa kaptura, na kadhalika? Huwezi kuwaacha? Huwezi kuwaacha?" Akasema, "Watu wanakuona kama mwonaji kutoka kwa Bwana. Mbona usiwaambie jinsi ya kuona maono?"

87 Nikasema, "Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawajui ABC zao?" Na kadiri unavyozidi kuhubiri, ndivyo wanavyozidi kuwa wabaya. Kwa hiyo, unaona, mfumo wote umeoza, unaporomoka. Hivyo tu.

88 Mungu hatauokoa ulimwengu kwa madhehebu fulani ama kwa mfumo fulani. Yeye atauokoa kwa Roho Mtakatifu. Na Roho Mtakatifu ni Neno lililodhihirishwa. Ni ahadi za Mungu zilizodhihirishwa. Naam, bwana. Tumechukua mapokeo yetu na kulitangua Neno la Mungu, kama tu walivyofanya katika siku alizokuja Yesu. Loo, naam, bwana!

89 Mungu aliahidi kutupa haja zetu, si matakwa yetu. Daima tunataka kitu fulani, bali tunakitaka kwa njia yetu wenyewe. Unasema, "Vema, na—nataka hicho. Mimi. . .Naam. Vema, Bwana, tutumie *hiki* na ututumie *kile*." Mungu anajua mahitaji yetu. Hiyo ni kweli kabisa. Yeye anajua hitaji letu.

90 Vipi kama mvulana wako mdogo alikuona ukinyoa kwa—kwa wembe wako wa kawaida, na angesema, "Baba, ninataka wembe huo"? Unajua si vizuri kumpa mtoto huyo wembe huo. Vema, vipi kama yeye angesema, "Baba, nilikuona ukifanya jambo hilo"? Vema, hilo ni tofauti. Wewe ni mtu mzima. Unajua jisni ya kutumia wembe. Wewe ni mtu mzima. U—u—mejawa na akili, kujua jinsi ya kutumia wembe.

91 Halafu basi, mara nyingi, tunaona Wapentekoste wakimwona mtu fulani akinena kwa lugha, ama kitu fulani kikifanya ibada ya uponyaji, na mfumo wetu wote unapotoka kwa kundi la waigaji wa kimwili wakijitokeza. Wanawaona wengine wakifanya jambo hilo, lakini huenda Mungu hakukuita kufanya jambo kama hilo. Na jambo hilo linafanya nini? Linasababisha uigaji wa kimwili, jambo ambalo linaleta lawama juu ya huduma ile ile iliyotumwa na Mungu. Ni kitu gani kinachosababisha jambo hilo? Mifumo.

92 Kama Assemblies of God lina mtu huko nje anayefanya jambo fulani, na Mungu yuko pamoja naye, na amethibitishwa, tunaliona hilo jinsi hiyo, ndipo makundi hayo mengine yanajitahidi kumpata mmoja, pia.

93 Angalia mfano ule mdogo, si muda mrefu uliopita, wakati mfumo wa "Daudi kadogoo" ulipotokea. Unaona? Na kila kanisa ilibidi liwe na Daudi kadogoo, wasichana wadogo wahubiri na wavulana. Na ilikuwa ni kitu gani? Kulinganisha, mlingano,

wakijaribu kuiga. Hilo ndilo lililotuingiza katika machafuko tuliyo nayo sasa. Hiyo ni kweli kabisa.

94 Ni kitu gani kilichowafanya ninyi Assemblies of God kurudi kwenye madhehebu wakati ambapo huo ndio mfumo ule ule ambao Mungu aliwatoa kwake? Mlijaribu kujilinganisha na Wamethodisti na Wabaptisti. Ni kitu gani kilichowafanya ninyi wa umoja, mkiwa na "hoja mpya" yenu, ni kitu gani kilichowafanya muunde madhehebu, kitu kile kile alichowatoa kwake? Jambo lile lile. Mnaendelea tu kufanya jambo hilo, tena na tena, na kurudia tena. Hivi hamwezi kuona si la Mungu? Kitu hicho chote kimeoza na ni makosa. Mungu hawaiti kwa chapa yenu ya kimadhehebu. Yeye anawaita kwa Kuzaliwa kwenu. Hakika. Hivyo ndivyo jinsi Mungu anavyowaita.

95 Mungu anajua mahitaji yetu, nasi hatuna budi kukubali jambo Hilo jinsi Yeye anavyoliweka. Si kulingana na mapokeo yetu, hatuwezi kamwe kulipokea namna hiyo, maana Mungu hatalipokea. Mungu hatakuwa na uhusiano wo wote na jambo hilo.

96 Tu—tunaona wengine. Mnasema, "Unaona, mtu fulani, mimi. . .Ndugu Branham, ninaona mtu fulani anayeweza kufanya jambo *hili*, na wengine *lile*. Utukufu kwa Mungu, Bwana!" Jamani! Kama Ndiye aliyelifanya jambo hilo, Ndiye atakayelifanya. Kama Yeye alikuitia hilo, haitakubidi kumwambia mtu ye yote habari hiyo. Litajionyesha lenyewe. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini tunataka kuwa kama akina nanii, jinsi ambavyo tumejiingiza kwenye mfumo tulio ndani yake sasa.

97 Sasa—sasa tunaona, katika siasa zetu za kimadhehebu, nasi tumekubali siasa, na kuacha siasa ziwaongoze wahudumu wetu, siasa za dini ziwaongoze wahudumu wetu, badala ya Roho Mtakatifu kuwaongoza wahudumu. Hiyo ni kweli. Mtu fulani anaona Kweli fulani ambayo anaamini, hawezi kuiendea, kanisa lake litamfukuza sasa hivi. Unaona? Kwa hiyo, unaona, unamwacha mwanadamu aongoze badala ya Mungu kuongoza, kwa maana mafundisho yako ya sharti ya kanuni zako za imani na kadhalika, linamweka mtu mbali nalo. Mmethodisti angewezaje kutoka na—na ahubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu? Ninyi wahudumu wa Kimethodisti mliopo hapa, ninyi wahudumu wa Kimethodisti, mngewezaje kufanya jambo hilo? Ninyi Wapresbiteri mngewezaje kufanya jambo hilo na mbaki kwenye kanisa lenu? Watawafukuza. Mnajua jambo hilo. Kweli, watawafukuza. Na ninyi, Wapentekoste, ni wabaya vivyo hivyo. Hilo ni kweli kabisa. Mradi tu ni mfumo fulani, ni mfumo fulani. Mfumo wote umeoza. Basi achaneni na jambo hilo, hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya kabla halijarudi.

98 Huenda usiamini jambo hilo, bali haya yanarekodiwa. Usikilizeni, miaka michache tangu sasa, kama kuna kitu kama

hicho, nanyi mtajua kama ni kweli ama si kweli. Siku moja, wakati nuru za jioni zitakapochomoza, utakuwa umechelewa kupita kiasi wakati huo, utasema, "Vema, huenda mtu huyo alikuwa anasema kweli." Bali umeishachelewa sana wakati huo.

99 Ni vile hasa Yesu alisema wakati alipokuja duniani. Alisema Mungu alikuwa amekwisha tuma kwenu hao manabii katika nyakati zote zilizopita, kila wakati ambapo mfumo wa—wao wa ulimwengu ungeporomoka, mfumo wao wa dini. Kasema, "Mlimfanya nini? Mungu aliwapelekea nabii nanyi mkamzika kaburini. Kweli kabisa. Halafu yapata kizazi kingine, mnaamka na kutambua ya kwamba huyo alikuwa ni nabii. Halafu mnafanya nini? Mnapamba hilo kaburi." Mnafanya nini? Mnayafanyia maisha yake kuwa kanuni ya dini. Hivyo ndivyo Israeli ilivyofanya hasa, walikuwa wamemchukua nabii Musa na kuyafanyia maisha yake kanuni ya dini.

100 Na hivyo ndivyo tunavyofanya. Martin Luther, John Wesley, watu wengine. Daima tunaangalia nyuma, unaona, tunaona mambo hayo. Nanyi mnayafanya maisha yao kuwa mapokeo ya dini, mnapamba makaburi yao. Na ujumbe wao ulikuwa wa siku zilizopita. Wakati mtakapoamka, vema, siku hiyo imepita tayari. Tuko katika siku nyingine. Mfumo wote ulifanya kazi hivyo, tangu mwanzo, mifumo ya kujibunia. Hakika.

101 Yesu, wakati alipokuja duniani, Yeye alikuja na akakuta kanisa na ulimwengu katika hali ile ile ilivyo siku hii. Ninaamini Yeye anakuja tena. Jinsi iyo hiyo. Ninaamini jambo hilo. Kuna kitu kimoja tu kinachoweza kuokoa jambo hilo, na hicho ni kule Kuja kwa Bwana. Hakuna kitu kinachoweza jambo hilo. Sijali. Sisi, Wamethodisti, hatutafanya jambo hilo. Ama, sisi, Wapentekoste, hatutafanya jambo hilo. Mungu atalifanya, katika kumtuma Yesu Kristo. Ninaamini ya kwamba Yeye atakuja kulingana tu na Maandiko. Atakuja, naam, bwana.

102 Kitu hicho chote kimekuwa madhehebu ya ki—kidini, kikiongozwa na madhehebu badala ya Roho Mtakatifu. Mifumo yetu ya elimu na madhehebu yetu yametuongoza katika njia nyingi sana mbali mbali, na, "Kuchukua mfano wa utauwa, na kukana Nguvu Zake," vile vile hasa Maandiko yalivyosema tungefanya. Nabii alisema, katika Timotheo wa Pili mlango wa 3, "Wakati unakuja wakati watu watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna."

Unasema, "Hao ni wakomunisti."

103 Hao ni wale wanaojiita ni Wakristo. Biblia ilisema, "Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake, hao nao ujiepushe nao. Kwa maana katika hao wamo wale wajiingizao katika nyumba za watu, na kuchukua mateka wanawake wajinga, waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi, wasioweza

kujifunza wala kuufikia ujuzi wa Kweli. Lakini kama vile Yambre na Yane . . . ”

104 Kumbukeni, walifanya vivyo hivyo hasa. Walikuwa—walikuwa ni waigaji. Kitu hicho kimeupiga ulimwengu wa Kipentekoste kama vile kilivyopiga hao wengine. Waigaji! Wakati Musa alipoitupa ile fimbo chini, Yambre na Yane walitupa fimbo chini. Musa alipoagiza vitu, nao wakaagiza vitu. Igizo la kimwili! Nawe utaepukaje jambo hilo? Hao si Wamethodisti, Wabaptisti, Mpresbiteri. Hao ni Wapentekoste, maana hata hawaninii—hata hawafikii kwenye kingo, hata kidogo, huko nje, hao wengine. Unaona? Nabii alisema ingetukia. Utalizuiaje lisitukie? Biblia ilisema hivyo. Hakuna Neno la Mungu litakalopata kushindwa. Ni Neno la Mungu, kwa hiyo jambo hilo limetufikia. Tunaliona mbele zetu. Amkeni, enyi watu, kabla ya kuchelewa sana.

105 Je! unategemea mfumo wo wote, mhemko wo wote, itikadi yo yote? Ambatana na Mungu, na Mungu pekee. Nenda kule, mpaka maisha yako yatakapobadilishwa na unakuwa ni kiumbe kipya katika Kristo. Mungu atashughulikia hayo mengine, Yeye anakutaka wewe ufanye jambo lo lote. Yeye, wewe mnaweza kuzungumza Naye basi, atakwambia. Usijaribu kulidhihaki, na kulifanya kama hao wengine. Kama *mtu* aliona nuru, na huyo *mwingine* akatetemeka mwili mzima, na huyo *mwingine* akafanya jambo lingine, usiyajali hayo.

106 Watu ishirini na watano waliinua mikono yao, jana usiku, kumpokea Roho Mtakatifu. Sijui ni wangapi. Kama kuna njaa hapo, hodi inapigwa hapo moyoni. Kila mmoja wenu anapaswa kumpokea Roho Mtakatifu papo hapo ulipokuwa unaketi, wakati moyo ulipoona njaa. Mungu anataka na zaidi kukupa Huyo kuliko vile wewe unavyotaka kumpokea. Kamwe huwezi kumaliza baraka za Mungu. Huwezi kamwe kumaliza wema wa Mungu. Huwezi kufanya jambo hilo.

107 Ungeweza kuwazia kijisamaki, urefu wa inchi moja na nusu, huko katikati ya bahari, kikisema, “Afadhali ninywe maji haya kwa uangalifu kwa maana siku moja huenda yakaisha”? Ungeweza kuwazia panya kwenye yale maghala makubwa sana ya Misri, akisema, “Nitakula punje moja kwa siku, na nijipimie, nijipimie mwenyewe, kwa sababu huenda nikaishiwa na chakula kabla ya mavuno yajayo”? Vema, hicho kingekuwa ni kichekesho.

108 Pia ni kichekesho zaidi kuwazia ya kwamba ungeweza kumaliza kila neema ya Yesu Kristo, na Nguvu Zake, na shauku Yake. Ameliandika katika Neno. Amekuahidi hayo. Nasi tuko hapa, asubuhi ya leo, tukiangalia kitu hicho wazi wazi.

109 Lakini unapoona baraka za Mungu zikijaribu kuwafikia watu Wake, na kuona kwamba wamevuruga sana kila kitu hivi kwamba, Yeye hawezi kuja kwenye mchafuko kama huo na

kulileta Neno Lake. Hatafanya jambo hilo. Hivyo tu. Chombo hi—hicho hakina budi kusafishwa vizuri kabisa. Tunapofika miongoni mwa Wapentekoste, tunaona wanawake waliokata nywele zao! Je! unajua hata haikubaliwi kwa mwanamke kuomba wakati amekata nywele zake? Nini ilitukia? Mama yako asingefanya jambo hilo, hata kidogo. Nini kilitukia?

110 Mna ricky fulani nyuma ya mimbara. Mna maskini kitu fulani kilichofundishwa kutoka kwenye shule ya Biblia iliyompeleka mbali zaidi na Mungu kuliko vile angaliweza wakati wo wote kumfikia Mungu. Mnakwazika juu ya urahisi wa Mungu. Kweli. Unafanya nini? Unapopata shahada ya juu, hiyo ina maana kwamba uko mbali kiasi hicho na Mungu. Unapopata Ph. D., LL.D, ama B.A. ya Sanaa, wewe uko tu umbali huo na Mungu. Mfumo wa elimu unakupeleka mbali na Mungu.

111 Elimu imekuwa ni wazo la Ibilisi. Hekima ya ulimwengu imekuwa ndilo wazo la Ibilisi, tangu mwanzo, kwa Hawa. Na huko nyuma kote katika wakati, ilijaribu kubadilisha imani rahisi katika kuamini Neno la Mungu. Laiti Hawa angaliamini tu Neno la Mungu, badala ya kujaribu kupata hekima zaidi. Alichukua ujuzi wake wa seminari kule, naye akavunja vizuizi, naye akapata . . . akamwacha Mungu. Na hivyo ndivyo seminari zetu za theolojia na kadhalika zinavyofanya. Inachukua mapokeo ya—ya mambo yaliyo nyuma ya jambo hilo.

112 Mungu ni mrahisi. Yeye ni mrahisi sana, yeye anapita juu ya akili za watu. Ni siku ya jinsi gani tunayoishi! Tunahitaji kumrudia Mungu, basi.

113 A-ha! Kubali, "Tunafikiri . . ." Naam. Na je! inambidi Mungu kutukubali katika mapokeo hayo? Bila shaka hatafanya jambo hilo. Hajapata kufanya jambo hilo. Mungu kamwe hajawahi. Ninataka mwanahistoria fulani anikemee kama ndivyo ilivyo, aniambie ni wapi.

114 Mtu fulani alitumwa duniani na ujumbe kutoka kwa Mungu, na baadaye, mara alipotoka nao, alijifunganisha na kundi la watu na kuunda madhehebu. Na madhehebu hayo yakafa. Hayakufufuka tena. Mungu aliyaweka kwenye rafu. "Yakawa," kama maskini yule mhudumu alivyosema jana usiku, "idadi, siyo Roho." Je! Wapresbiteri waliinuka? Je! Wakatoliki waliinuka kutoka kwenye lile Baraza la Nikea?

115 Kanisa la kwanza la kipentekoste lilikuwa ni pale—pale pentekoste. Ama, ninamaanisha, Kanisa kamwe halikuanzia Rumi, kwenu ninyi Wakatoliki. Ninataka mtu fulani anionyeshe mahali ambapo Kanisa lilianza huko Rumi. Madhehebu yalianza huko Rumi, kilicholiua Kanisa. Bali Kanisa lilianzia kule Yerusalemu, si Nikea. Unaona? Bila shaka.

116 Tulianzia wapi? Unaona? Unapata . . . Mungu atamtuma mtu fulani na ujumbe, naye atamalizia na kupata sifa kwa vitu

mbali mbali, na kichwa chake kinaingia kiburi, kisha anaunda madhehebu. Basi Mungu anayaweka moja kwa moja kwenye rafu kama alivyolifanyia kanisa Katoliki, na sisi sote tumeketi humo, ambalo ni mama wa kitu hicho chote. Na sasa mfumo wetu unaporomoka.

117 Loo, tunaishi kwenye wakati wa jinsi gani: naam, kuukataa Ujumbe Wake, kukataa ahadi Zake, kukataa wale waliotumwa na Kweli. Tunataka Mungu afanye jambo lile lile katika siku zetu, kama tu vile a—alivyofanya wakati huo. Tuna shauku yake, lakini basi tunajikuta tumechafuliwa kabisa, siasa tupu, wadhehebu wamechafuliwa kabisa na upotovu wa mawazo ya kujibunia. Nami nina lundo la vitu vilivyoandikwa hapa chini ambayo sipaswi kuvisoma. Nafikiri nitayaachilia tu.

118 Angalia, sasa, rudini kwenye Kweli ya Neno. Mungu anaishi peke yake. Mungu anawataka watu Wake waishi peke yao pamoja Naye. Hawatakuwa wamejifunganisha na cho chote, mihemko yo yote, mapokeo. Anataka watoto wanaotii Neno Lake. Yeye anaweza kuweka Neno Lake hapo ndani. Mungu alisema, Yesu alisema, "Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, basi ombeni mtakalo." Aidha hiyo ni Kweli ama si Kweli. Kama ni Kweli, itatenda kazi.

119 Sasa, je! unataka kujua siri inapolala, nguvu za maono na kadhalika? Ni kurudi kwenye Neno. Ni Neno la Mungu. Yesu alikuwa ni Neno. Yeye alikuwa ni dhihirisho la Mungu. Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa Nafsi Yake. Naye alikuwa ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno. Naye Neno alifanyika mwili."

120 Na Neno linataka kufanyika mwili wetu. Lakini wakati tuwapo sote tumefungwa katika kila namna ya upuuzi, na mapokeo, na kuachiliwa kuishi kama ulimwengu, na vitu kama hivyo, halafu tumtarajie Mungu kufanya jambo hilo? Mbona, bila shaka hatafanya, sijali tunaiga mambo mangapi.

121 Inafikia mahali, mpaka, ndugu, jambo fulani linakaribia kutukia. Sitaki kuwaumizeni. Ninataka kuwabariki. Sikilizeni. Moja ya siku hizi, Kunyakuliwa kutatukia, na Bibi-arusi atakuwa ameenda, nanyi hamtajua jambo lo lote juu yake. Hata hawatajua Neno moja juu yake.

122 Kila mtu anakubali, akisema, "Loo, moja ya siku hizi, Yesu atashuka kutoka mbinguni, na kusema, 'Njoni, ninyi Wapentekoste wote, ama ninyi Wabaptisti,'" na mawazo yetu ya kimapokeo juu ya jambo hilo. Haitakuwa hivyo.

123 Maoni yangu ndiyo haya. Siku moja wakati Yesu alipokuwa. . .ilikuwa imetabiriwa ya kwamba Yesu angekuja duniani. Naye akaja, akaishi, akafa, hakuna mtu aliyejua lo lote juu yake, hata kidogo. Si hata asilimia moja ya Wayahudi walijua Yeye alikuwapo duniani. Ni mmoja kati ya mia moja aliyejua Yeye alikuwapo duniani.

124 Yohana Mbatizaji; kutoka Isaya, kutoka Malaki, mbona, wakati walipotabiri juu yake, walisema, "Milima yote, mahali palipoinuka, patashushwa. Mahali pote paliposhushwa patainuliwa. Na, lo, jinsi kondoo dume . . . Ma—majani yatapiga makofi, na milima itaruka kama kondoo dume wadogo," mambo yote hayo. Vema, hao watu wa desturi walikuwa wameyawazia kichwani yote, kwa njia nyingine. Naye huyu hapa Yohana akaja na kuhubiri vile vile hasa Yeye alivyosema, na hata wanafunzi hawakujua jambo hilo.

125 Siku moja walimjia. Akasema, "Mwana wa Adamu yuaenda Yerusalemu."

126 Akasema, "Vema, ni kwa nini basi, kwamba Maandiko yanasema, waandishi wanaandika na kutwambia, ya kwamba, 'Kabla mambo haya hayajatukia, ya kwamba Eliya atakuja'?"

127 Akasema, "Tayari amekwisha kuja, wala hamkutambua." Na ndipo akawaambia ilikuwa ni Yohana. Lakini akasema, "Yeye alifanya yale tu ambayo Maandiko yalisema angefanya, nao wakamtendea yale ambayo Maandiko yalisema." Unaona?

128 Moja ya siku hizi, mtashangaa, wakati huo Unyakuo utakapokuja. Kumbukeni, kuna kama watu mia tano, mia nane wanaokosekana kila siku, duniani kote, ambao hawawezi kujua kilichowapata. Naye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, vivyo hivyo ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, ambapo watu wanane waliokolewa."

129 Moja ya siku hizi, hukumu itaipiga dunia, italipiga taifa hili, italipiga kanisa, ikiusafisha kwa ajili ya ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu unaokuja. Basi ndipo utasema, "Vema, kwa nini lilisema ya kwamba Unyakuo utakuja kwanza kabla ya mambo haya kutukia?"

130 Yeye atasema, "Kumekwisha kuja wala hamkutambua." Naam. Mtu fulani akienda zake kanisani; maskini bibi fulani akienda mahali fulani kusalimia; wametoweka. Hamjui wakati gani jambo hilo lilipotukia. Limewapita. Imekuwa hivyo mara zote. Vivyo hivyo ndivyo itakavyokuwa hivyo tena.

131 Amkeni, enyi Wapentekoste. Tikiseni dhamira yenu. Tambueni saa mnayoishi. Hii ni saa nzito sana. Ninyi watu, jinsi mnavyowafanya watu wenu wafanye na kuenenda, na—na kadhalika. Na ilikuwa ni kawaida kwamba, mliona aibu. Loo, ilikuwa ni aibu kwa Mkristo kwenda kuona sinema. Hawapaswi kufanya hivyo, hata kidogo. Ibilisi aliweka moja juu yenu. Aliweka televisheni moja kwa moja ndani ya nyumba yenu, na akawaletea sinema, kila namna ya upotovu, na cho chote kile, nanyi mnaruhusu jambo hilo.

132 Angalieni shule zetu. Angalieni ninii zetu . . . Huku nje, wasichana wadogo mitaani, wamejibana na kila namna ya nguo za kizinzi. Na—na hapa katika jiji la Chicago, kila siku

thelathini, kila—kila mwezi kuna visa thelathini elfu vya kutoa mimba vilivyoandikishwa, katika tu usajili mmoja.

133 Ni dhambi ngapi zilitendwa katika jiji hili jana usiku? Hivi hapakuwa ni mahali pazuri zaidi wakati mbwa mwitu alipobweka kote jangwani hapa, na Mungu akapaangalia, wakati maskini yule Hopi wa kale ama Navajo alipopitia hapa katika vichochoro vyake? Sasa angalia uchafu huu, na upotovu tu, na—na mapokeo na siasa. Na yote ni takataka za uchafu unaotiririka na unanuka katika pua ya Mungu. Ataninii . . . yamepotoka, mbele Zake.

134 Yeye ataulipua vipande-vipande, moja ya siku hizi. Naye ataipasua dunia, nayo itajifanya mpya kwa mlipuko wa volkeno. Ndipo utakuja Utawala wa Miaka Elfu basi, ambapo wenye haki watatoka watembee juu ya majivu ya watu waovu, kulingana sasa, na Malaki.

135 Kabla, sasa, kumbukeni, kabla ya jambo hilo halijatukia, hata hivyo, kuna jambo fulani linalotukia. Tutapata mtikiso kutoka kwa mjumbe fulani kabla ya kutukia jambo hilo, vema, sasa, Ujumbe wetu kwa siku yetu. Sasa angalia.

136 Tunaona, wakati wa kuja kwa Bwana Yesu, na wakati alipokuja katika siku Zake. Angalia katika siku Zake, wakati alipokuja.

137 Sasa tunaona ya kwamba Rumi ilikuwa ikitafuta mtu hodari sana mwenye kipaji cha kijeshi, masihi fulani, ambaye angekuja na kuwafukuza Wayunani watoke duniani, na hao wengine. Na—na anataka . . . Walikuwa na kiinimacho. Yeye alikuwa na kitu ambacho angewafanya hao wengine wote wajionee aibu. Walitaka mtu hodari sana mwenye kipaji cha kijeshi. Hicho ndicho walichotaka.

138 Israeli ilitaka nini? Masihi fulani. Wanataka masihi fulani, jemadari fulani. Walitaka jemadari aje, ambaye angewachukua na kuwafukuza Warumi wote, na kuwafukuza watoke nchini mle, na kuanzisha ule Ufalme kule Yerusalemu. Mungu alijua haja zao. Yeye aliwapa kitu gani? Mtoto Mchanga; Mtoto Mchanga, Mwokozi. Aliwapa Mwokozi. Wao walifikiri walikuwa wameokolewa, bali aliwapa Mwokozi.

139 Na hivyo ndivyo ilivyo leo. Kama angetuma cho chote kwetu, ingekuwa ni Mwokozi, wakati tunapofikiri ya kwamba tumeokolewa. Yeye alijua walichohitaji. Leo, angalia siasa zetu, jinsi zilivyopotoka, vile vile. Vipi kama—vipi kama Mungu angaliangalia leo?

140 Angalia Urusi. Urusi inalilia masihi fulani. Wanataka mtu fulani, m—mtu mwenye kipaji cha kisayansi, ambaye anaweza kuwapeleka mwezini kabla ya Marekani kuanza. Bila shaka. Mataifa mengine yote yanamtafuta. Wanataka mtu mwenye kipaji cha sayansi atakayewapeleka mwezini, anayeweza kuvumbua namna fulani ya bomu itakayowaangamiza wote,

iangamize mabomu yetu ya haidrojeni na kuwakomesha; nao wanaweza kuchukua mabomu yao wenyewe na kuyamimina juu ya kila mtu kabla mtu ye yote mwingine hajaanza, na ndipo watauteka ulimwengu wote mzima. Urusi inamtafuta Masihi wa aina hiyo.

141 Miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, Masihi wa kweli alisulibishwa. Aliahidi kurudi tena. Aliahidi Roho Mtakatifu angeangaza Nuru Yake tena, katika siku za mwisho. Sijui, kama akija, kama tungekuwa tu kama Wayahudi walivyokuwa katika siku ile. Kama tunaangalia, kanisa linatafuta masihi wa aina gani?

142 Baptisti linatafuta ki—kitu fulani kikubwa kidogo zaidi kuliko Billy Graham, ambaye anaweza kuwachukua Wamethodisti wote, na Wapresbiteri, na—na Wapentekoste, aseme, "Ninyi nyote fumbeni mdomo. Nitafanya shirika moja kutokana na ninyi nyote."

143 Wapentekoste wanatarajia nini? Wanamtafuta mtu mwenye kipaji ainuke, ambaye anaweza kuwafanya wote kuwa Waasemblies. Na wa—wa umoja wanamtafuta wa umoja fulani ambaye anaweza kuwafanya wote kuwa wa umoja. Kanisa la Mungu linamtafuta mtu, atakayewafanya wote kuwa kanisa la Mungu.

144 Mnafanya nini? Mnatengeneza shule za Biblia na kuwaelimisha; na kuwatuma wengine, ambao Mungu angewatuma, mbali sana Naye kuliko walivyokuwa hapo mwanzo. Ninajua hamkubaliani na jambo hilo, wengi wenu. Lakini kitu cho chote . . .

145 Mama yangu alizoea kutwambia. Wakati tulipokuwa watoto, tulilelewa maskini sana; tulichemsha ngozi za nyama na—na kupata mafuta, kuokea mkate wetu wa mahindi. Na kila Jumamosi usiku ilitubidi ku—kunywa kipimo cha kastoroli. Si—sisi, ninii yetu . . . Tulikuwa na, karibu, ugojwa wa ukosefu wa mlo kamili, kula kiasi fulani, kula chakula kile kile, cha majani mwitu, na kadhalika. Naye mama . . . Nilikuwa nachukia kitu hicho. Ningali ninakichukia, bado, leo, ninapoenda kuyanywa. Ningeziba pua yangu, na kusema, "Mama, siwezi kuyanywa. Yananitapisha. Yananitia kichefuchefu."

146 Akasema, "Kitu cho chote kisichokutia kichefuchefu hakitakufaa kitu."

147 Hiyo ndiyo shida ya kanisa la Pentekoste siku hizi. Hamtaki kusikiliza kitu ambacho kita—kitawafaa. Kitawachefua kwenye mapishi yenu ya theolojia, bali kitawafaa. Kitawatoa, kiwarudishe kwenye Neno la Mungu, na kuwarudisha kwenye Imani iliyotolewa mara moja kwa watakatifu; na kuwaondoa kwenye shule zote hizi hapa za Biblia, semina ya theolojia, na zinazowapa wahudumu kila namna ya digrii. Mungu kamwe hakusambaza matofaa kama hayo yaliyo na chachu. Yeye

anawataka watu wawe na Imani, waamini yale yaliyoandikwa tayari. Huna haja ya kujilundikia kitu kingine.

148 Ninajua hilo ni gumu. Mimi siko hapa kuwabembeleza, na kuwafanya mcheke, na kuwafanya mpige makelele. Niko hapa kuwaambia Kweli katika Mungu. Nanyi mtaona, siku moja, kama hamwamini Hilo hivi sasa. Siku itakuja wakati mtakaposema, "Hiyo ilikuwa ni kweli." Kweli. Inawabidi kurudi.

149 Kitu hicho chote kiko katika hali hii. Hakuna kitu kilichosalia cha jambo hilo, kitakachokuja, ila Kuja kwa Bwana Yesu. Wala hatakuja kwa Assemblies of God. Hatakuja kwa Baptisti. Yeye atakuja kwa kila mtu binafsi. Hiyo ni kweli.

150 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Na mara hiyo Nuru ilipogusa hiyo Mbegu, [Ndugu Branham anadata kidole chake mara moja.] walikuwa kwenye Uhai namna *hiyo*.

151 Angalia hao wanatheolojia wakisimama kule, walipomwona akitambua mawazo yaliyokuwa moyoni mwao. Walikuwa wameisha ona uigaji mwingi wa kimwili, hapo nyuma, nao wakasema, "Mtu huyu ni Beelzebuli, mpiga ramli." Hao walikuwa ni wanatheolojia.

152 Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu, Ibiilisi, na kazi zake mnazifanya."

153 Bali maskini kahaba mmoja alipoenda pale, chini kule, kwenye kile kisima kule Samaria. Basi Yesu akamwambia, "Nenda, kamwite mumeo."

Akasema, "Sina mume."

154 Akasema, "Umesema kweli. Ulikuwa na watano, naye unayeishi naye sasa si wako."

155 Akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe u nabii. Tunajua, Masihi ajapo, Yeye atafanya mambo haya."

Akasema, "Mimi ndiye, ambaye ninasema nawe."

156 Ilikuwa ni kitu gani? Ile Nuru iligusa hiyo mbegu ndogo iliyochaguliwa tangu zamani, na upesi ikapata Uhai. Ni tofauti jinsi gani na hao wanatheolojia, wote wana kasumba!

157 Akakimbia mjini, akasema, "Njoni, mtazame Mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda. Haimkini hii kuwa ndiyo ile ishara yenyewe ya masihi tunayoitarajia?"

158 Nao madaktari wa theolojia walisimama pale, wakasema, "Yule jamaa ni Beelzebuli." Unaona, hawakuweza kueleza jambo Hilo. Hawakuwa na njia ya kulielezea. Kwa hiyo ilibidi wajibu kusanyiko lao, kuwapa namna fulani ya wa—wazo la siasa kali.

159 Jambo lile lile limewasili tena, na watu hawataamini. Watu hawataamini. Makanisa hayataamini. Si ajabu. Huwezi kusikitishwa nalo, kwa maana Biblia ilisema hawataamini.

Lakini ni ninyi watu binafsi, ninyi mliochaguliwa kuupata Uzima. Angalieni hudumani sasa na mwone tunaishi saa gani. Huikeni. Hebu Uzima uliokuwa katika Kristo na uingine ndani yenu, moyoni.

Ulisema, "Loo, nafikiri. Nafikiri jambo *hili*. Na . . . "

160 Huna wazo linalokuja. Acha mawazo yaliyokuwamo ndani ya Kristo yawe ndani yako, na hilo ni Neno. Hiyo ni kweli. Wazia mawazo aliyowazia Yeye.

161 Sasa, sasa, sijui, leo, Marekani. Sitawaweka muda mrefu zaidi. Marekani, mmekuwa mkilia kwa sauti kuu kuliko wote. Mnataka nini? Ninakuja nyumbani sasa kutoka nchi za ng'ambo. Mnataka nini? Mnataka mtawaliwe na kitu gani? Mnataka mtu mwenye kipaji cha elimu, ndiye mnayemtaka. Nanyi mnaye. Sitaki kuwaudhi. Nataka kuwaambia Kweli. Mnaye, hata ingawa iliwabidi kuunda mashine danganyifu za kupigia kura. Mmempata. Marekani, mmeegemea sana kwenye elimu, si Biblia; kwenye elimu.

162 Makanisa yamejengwa sana juu ya theolojia ya kielimu, mfumo fulani wa kujibunia, kanuni za imani. Nao Wapentekoste wamezolewa moja kwa moja kwenye kitu kile kile, kama tu mbao zilizopwelewa majini, zikielekea kwenye bwawa la maji. Sawa. Mnataka kanuni ya imani. Hamtaki Ukweli.

163 Sasa angalia. Mlifanya nini? Kila kitu kilikuwa eli- . . . Mnaitaka vizuri sana, hata mkatoa televisheni yenu, na kumweka Bw. Nixon na Bw. Kennedy humo, kuchunguza akili zao kabla hamjafanya jambo hilo. Halafu, hata kuna watu wazuri wa kutosha waliosalia Marekani wasingefanya jambo hilo; wanajua urithi wetu. Tunajua sisi ni wa wapi.

164 Na ninyi wanachama wa Demokrat! Mimi si Mdemokrat wala Mrepablikan. Mimi ni Mkristo. Lakini ninyi, Wanademokrat, ambao mngeruhusu maskini Ricky mdogo fulani aje, nanyi mngeuza haki zenu za mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya siasa zenu, na kupigia kura kitu ambacho taifa letu lilianzishwa lipate kukikimbia, hamna aibu. Mmempata Ahabu yule yule na Yezebeli!

165 Ninyi wanawake wa Kimarekani mlitaka mtindo. Mna ninii . . . Haiwabidi kwenda huko Paris sasa. Mnao papa hapa, Mfaransa halisi, atakayewapa huo. Mna mtindo maji-maji wa kukata nywele, na mitindo yenu yote na kadhalika, ambayo mnataka kufuata. Mmepata kile hasa mnachotaka. Yeye atawaelekeza wapi? Moja kwa moja kurudi Urumi, ndiko alikotoka hasa.

166 Na ninyi Waprotestanti, mnataka shirika fulani kubwa la kuwaongoza, liwapelekeshe, liwatawale. Mtalipata, ninyi, Baraza la Makanisa Ulimwenguni. David duPlessis anawezaje, rafiki yangu, daima, kwenye baraza hili la ekumeni analonena habari zake, na kuwaleta hawa Wapentekoste kuwaingiza humo?

Hivi mna nini ninyi Wapentekoste, mnaopiga makelele juu ya, "Dk. Baba Mtakatifu *Fulani* karibu"? Loo!

167 Unajua Biblia ilisema, "Usimwite mtu ye yote, 'baba.'" Hivi mna nini? Hayo ni mafundisho ya Bwana wetu. Kuna nini? Je! hamwijui Biblia yenu? Je! hamumjui Bwana wenu? Roho Mtakatifu asingewafundisha kufanya jambo kama hilo.

168 Je! hamtambui ya kwamba wakati hawa Wapresbiteri, Waluteri na kadhalika wanapojaribu kuingia, kutafuta Hayo, ni wakati wa mwisho? Hawaingii. Biblia ilisema hawakuingia. "Walipokuja kutafuta Mafuta, Bwana Arusi akaja; walipoenda kutafuta Mafuta." Basi ni vipi kuhusu Kunyakuliwa sasa? Unaona? Biblia ilisema, ya kwamba, "Wakati wale wanawali waliolala walipokuja kununua Mafuta." Ni wangapi wanajua kwamba hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Wakati wanawali waliolala walipokuja kutafuta Mafuta, Bibi arusi akaingia ndani." Hawakuyapata.

169 Walirudi, nao wakatupwa katika giza la nje. Unaposikia uvumi huu kuhusu Wamethodisti kadha, Wapresbiteri, Wabaptisti; mna nini? Amkeni. Muda umepita mno kuliko mnavyodhania. Walirudi. Lakini huenda ikawa walikuwa na mhemko, bali hawakuwapo Kule. Kumbukeni, walikuwa kwenye giza la nje.

Labda unasema, "Jambo hili litatukia lini?"

170 Alisema, "Huenda limekwisha kutukia, moja ya asubuhi hizi, wala usingejua ni kwa nini, ni vipi." Ninatumaini unaweza kusoma. Ninatumaini unaweza, una Roho wa Kristo kutosha kujua ninalozungumza habari zake, Roho Mtakatifu akufunulie jambo hilo. Hizi zinarekodiwa, na zinaenda ulimwenguni kote. Unaona? Bali unatambua.

171 Siku chache tu zilizopita, wakati hao Malaika saba waliposhuka katika lile ono. Wengi wenu wakijua jambo hilo. Kasema, "Ondoka uende Tucson na ungojee kule kwa muda, nawe utasikia mlipuko ukilipuka. Utakapolipuka, rudi huku. Na ile Mihuri Saba ilifunguliwa pale maskanini, hivi majuzi. Nilipowaona watu wakija, wakisimama kule, tangu saa tisa usiku, kusudi wapate nafasi, wapate kuingia kwenye ukumbi, na kadhalika. Kuona mioyo yenye njaa kutoka kila mahali. Nilifikiri, "Ee Mungu, hatuna budi tuko katika wakati wa mwisho sasa." Kumbukeni, "Kupiga baragumu kwa Malaika wa saba, siri za Mungu zilitimizwa." "Kisha akaja Malaika kutoka Mbinguni, na akaapa huku ameinua mikono yake kutoka Mbinguni," Ufunuo 10:1 hadi 7, "ya kwamba hakutakuwa na wakati baada ya haya." Kweli kabisa, ile saa.

172 Yeye anakuja kwa kanisa gani? Kanisa tunaloishi ndani yake, Wakati wa Kanisa la Laodikia, wakati wa mwisho wa kanisa, wakati uvuguvugu, wa kutosha tu kucheza-cheza, kusema, "Ndiyo, nimempata. Nilinena kwa lugha. Nilipiga

makelele. Haleluya. Nimempata." Na kurudi makanisani mwetu, wanaonekana kama kundi la Mayezebeli, wanaonekana kama kundi la sijui ni kitu gani, upotovu. Hebu kumbuka, upande wako wa nje unaonyesha upande wako wa ndani. Haidhuru ushuhuda wako ukoje, maisha yako yananena kwa sauti kuu kuliko maneno yako. Loo!

173 Tuko hapa. Tumefika. Jambo fulani liko karibu kutukia. Linatoka huko Juu, si kutoka kwa moja ya vitu hivi hapa. Linatoka Juu. Mungu atamtuma Kristo. Amina.

174 Naam, tuna mtu wetu mwenye kipaji. Yuko wapi? Sasa mnataka mtu mwenye kipaji, ulimwengu wa kanisa. Simaanishi ninyi watu binafsi hapa. Huu unarekodiwa. Vipi basi? Mnamtaka. Mtampata, mtaingia moja kwa moja kwenye baraza la makanisa, kitu kile kile mlichotoka kwacho, mpate kuwa jinsi mlivyo. Halafu tena madhehebu yenu yanawarudisha moja kwa moja ndani yake mahali, mahali pale pale mlipotoka, kitu kile kile Mungu alicholaani, ule upotovu, uchafu na kinyaa. Mbona, katika baraza hilo la makanisa, baadhi yao hata hawaamini katika kuzaliwa kibikira, Kuja kwa Kristo, wala cho chote kile. "Basi watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana?" Haya basi.

Vema, wakati wangu wa kuondoka, nafikiri, umefika.

175 Ndugu ama dada, hebu kumbukeni tu jambo hili, tuko wakati wa mwisho. Elimu imechukua mahali pa wokovu. Kanisa la kimadhehebu limechukua mahali pa ule Mwili na pa Bibi-arusi wa Kristo. Kuketi katika upotovu huo wote, hivyo ndivyo mnavyotaka. Hivyo ndivyo watu wanavyotaka. Hivyo ndivyo ilivyo katika kanisa la Kimarekani. Hivyo ndivyo ilivyo katika Upentekoste. Wanataka mtu aje na asiwaambie Ukweli. Hawautaki. Hebu uwaambie; wao watasema, "Si lazima nisikilize upuuzi kama Huo," wanainua pua yao ndogo juu na kutoka humo jengoni. Hawatausikiliza. Kwa nini? Hicho ndicho kilicho moyoni mwao. Wanaonyesha waziwazi kile walicho hasa. Ni yupi kati ya wale manabii aliyewahi kuja katika zile siku za kale? Kristo alikuja wakati gani? Ni mjumbe gani aliyewahi kushuka kutoka Mbinguni ila yule ambaye kanisa lilimkataa? Tuko hapa. Ulimwengu unaporomoka. Kanisa linaporomoka. Mifumo inaporomoka. Kwa nini? Kwa maana ni mfumo ulio nje ya Mungu. Jambo ndilo hilo. Tuko—tuko kwenye wakati wa mwisho. Hakuna jambo lingine lo lote linalowezea kufanyika. Naam, bwana. Kila kitu, kumbukeni.

176 Hebu na tuulize swali hili kabla hatujaendelea. Vipi—vipi kama Urusi ingelimpata masihi wake? Ni kitu gani kingetupata? Unaona? Tunakumbuka hilo vizuri sana, Ujerumani ilimpata wake, si muda mrefu uliopita. Tunakumbuka jambo hilo vizuri. Walipata masihi wao, Hitler wao, mtu wao mwenye kipaji. Vipi kama Urusi ingelipata wake, ingekuwaje? Kama kusingekuwako

na Mungu wa rehema Mbinguni, sijui tungefanyaje, na matumaini yetu yangekwisha.

177 Kuna Kanisa la kweli. Kuna kanisa linalongoja kule Kuja kwa Bwana. Mungu sikuzote atatujalia jambo hilo, lakini ni wale tu waliokusudiwa. Unasema, "Itafaa nini kukubali, kama ni mfumo wa namna hii?" Kuna Mzao uliokusudiwa tangu zamani. Wakati Nuru hiyo itakaposhukia mzao huo, watalikaribisha namna *hiyo*. [Ndugu Branham alidata kidole chake mara moja—Mh.] Atachipuka. Watachanua, sasa hivi. Hakika.

178 Wengine watapita juu ya jambo hilo moja kwa moja. Wanaamini katika mfumo wao. Na hivyo ndivyo tu ilivyo sikuzote, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu. Waliamini jambo lilo hilo.

179 Wale waliokusudiwa Uzima wa Milele, waliupata. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu," alisema Yesu, "asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba watakuja." Inatupasa tu kutawanya Mbegu, kutupa Nuru. Loo, kila mmoja wenu anapaswa kuwa mnara wa taa.

180 Enyi Wapentekoste mnaodai kuwa mna nguvu sana! Enyi Wapentekoste mnaodai kubusu kikombe chenye mzingo wa dhahabu cha baraka za Kristo! Enyi wanawake mnaoweza kutoka kwenda nje hapa na kuruhusu na kufanya, na kuwaacha wahudumu wa kizazi hiki kuwakejeli na kuwaambia ni sawa kwenu kuwaacha watoto wenu wavae kaptura, na ninyi wanawake, mabibi, mnaokata nywele zenu. Basi hamjui Biblia ilisema ya kwamba mwanamke . . . Mwanamke anayekata nywele zake, Biblia ilisema mumewe ana haki ya kumtaliki. "Yuaaibisha." Zamani ilikuwa ni kosa. Kujipaka rangi? Kuna mwanamke mmoja tu katika Biblia aliyewahi kujipaka rangi usoni mwake, na huyo alikuwa ni Yezebeli. Naye Mungu akamlisha kwa mbwa. Kwa hiyo mnaona hicho kingekuwa ni nini, nyama ya kawaida ya mbwa. Kwa hiyo usininii—usininii . . . Hebu jitenge tu na mambo hayo. Hayo hayawastahili Wakristo. Naam.

181 Waambie jambo hilo. "Vema, mimi ni mfuasi wa Assemblies. Mimi ni mfuasi wa umoja. Mimi ni mfuasi wa *hili*." Hiyo ni kweli. Wewe ni mfuasi wa hilo. Lakini kama wewe ungalikuwa ni wa Kristo, ingekuwa ni kitu tofauti.

182 Wakati Neno la Mungu na Mbegu ya Mungu ilipokuwapo pale, ingechanua mfano wa Ukristo. Ingechanua kitu ambacho ulimwengu ungekicheka na kukifanyia mzaha, kama ulimwengu ulivyomfanyia Bwana wakati alipokuja, kama ulivyomfanyia kila nabii aliyekuja. Waliwacheka na kuwafanyia mzaha, na kuwatupa makaburini. Lakini ufufuo wa wafu unakuja. Ulimwengu huu, watu wanaweza kuishi kwa ajili ya ulimwengu huu, ulimwengu ujao. Inategemea mawazo yako yako wapi, hapo ndipo hazina zako zilipo pia. Hebu na ziwe ziko Mbinguni na

kwenye kule Kuja kwa Bwana. Uwe mfano wa uanamama. Uwe mfano wa uanaume. Kuwa mfano wa Mkristo. Ishi Maisha. Fanya yaliyo sahihi.

183 Watu siku hizi, hata wainjilisti wetu, ni matajiri sana. Kila kitu, inabidi waahidiwe kiasi fulani cha fedha na mambo makubwa makubwa, na kujenga majengo makubwa ya mashirika na vitu kama hivyo, kitu kile kile ambacho Wapentekoste waliacha. Tuko hapo, tumerudi papo hapo tena. Ni kitu gani? Yote yanameremeta na kung'aa. Unajua, kila kitu hakina budi kung'aa. Hollywood inawaka, naam, bali Injili inameka. Kuna tofauti kubwa kati ya kung'aa na kumeka. Ambapo ka—kanisa linawaka, ambayo ni mitindo ya Hollywood, makanisa makubwa kuliko yote, minara yake mikubwa kuliko yote, umati uliovalia nadhifu kuliko wote, na kadhalika, linawaka kwa mambo hayo, wafuasi walio wengi sana. Wabaptisti walikuwa, katika mwaka wa '44, "Milioni moja zaidi katika mwaka wa '44," chini ya Dk. Billy Graham na wengi wa hao.

184 Wakati nilipoketi kwenye kiamshakinywa cha Billy Graham, hapa si muda mrefu uliopita, kwenye jiji letu. Mtu huyo, mwinjilisti huyo, mtu mashuhuri wa Mungu! Ninamwombea, daima. Amelala kule, ni mgonjwa. Ninamheshimu. Yeye ni aina ya mwakilishi aliyeshuka kwenda huko Sodoma, na akawatoa hao watu Sodoma, kila mtu ambaye angeweza kutolewa.

185 Lakini, kumbukeni, Kanisa-Teule halikuwa huko Sodoma. Kulikuwa na Malaika aliyekaa kule milimani, pia, naye akawaonyesha ishara, lile Kanisa-Teule.

186 Lakini wakati alipofanya hivyo, akiwa amesimama juu kule, nami ninamwona amesimama pale, akasema, "Kuna nini hapa?" Akasema, "Mimi . . ." Akasema, "Huu hapa mfano." Kasema, "Mtakatifu Paulo alishuka akaingia katika mji, na akapata mwongofu mmoja. Akarudi, mwaka mmoja baadaye, alifanya nini, ilikuwaje? Alipata thelathini kwa huyo mmoja." Akasema, "Mimi ninaingia katika mji, ninapata waongofu elfu thelathini katika majuma sita. Ninarudi baada ya mwaka mmoja wala siwezi kupata thelathini. Kuna shida gani?" Akasema, "Ni ninyi wahubiri wavivu." Kasema, "Mnachukua kadi zenu za maamuzi, na kuketi huku mmeanika miguu yenu juu ya dawati mahali fulani, na kuwapigia simu." Na akaendelea. Nilimpenda mtu huyo kwa ujasiri wake.

187 Ninachukia kuona joga fulani, kibaraka fulani wa kimadhehebu. Na—napenda mtu, mtu aliyetumwa na Mungu anayeshindania imani yake, haidhuru nini. Inapothibitishwa kwamba amekosea, anakubali, kisha anarudi na kuanza tena. Hiyo ni kweli.

188 Naye alisimama pale na kuzungumza namna hiyo. Nami nikawazia. Nilikuwa nimeketi na Dk. Mordecai Hamm, ambapo,

yeye ni rafiki wangu msiri, ndugu wa Kibatisti. Nami nimemjua, loo, kwa miaka na miaka na miaka, nasi tumeshikiriana pamoja. Basi mimi na yeye tulikuwa tumeketi mezani, pamoja. Nikafika nyumbani kwake. Tukaenda kule pamoja. Tukaketi pale.

189 Nikawazia, "Loo, jamani!" Vipi? Si kuingilia wala kusema jambo lo lote juu ya mwinjilisti huyu mashuhuri. Lakini niliwazia, "Billy, ni nani kati ya wahudumu wa Antiokia, wakati Paulo alipoenda huko Antiokia na kumpata mmoja wa waongofu wake, ni mhudumu gani kule aliyemchukua mwongofu huyo, akamwingiza ofisini mwake, faraghani, na kumlisha na kuzungumza naye?" Hakukuwapo na hata mmoja. Kwa nini? Paulo alimchukua akampeleka mbali sana na mambo ya ulimwengu huu, loo, mpaka Mungu akathibitishwa na kuimarishwa moyoni mwake. Mtume huyo kamwe hakuiachilia nafsi hiyo iende, mpaka mtu huyo alipokuwa kweli amethibitika na kuimarishwa katika Kristo.

190 Na, leo hii, tunafanya nini? Tunawaleta hawa maskini wasichana wadogo, na wanaume na wanawake, wawe wafuasi wa makanisa, nao wanakata shauri, katika saa ya kukata shauri, na mambo kama hayo. Tunawaleta, na kuwatuma moja kwa moja huko nje, waende jinsi walivyo. Na ni nini? Wao hawajafikia mahali po pote, kwa vyo vyote. Hawakuwa na lo lote ila walishikwa na mhemuko mdogo, kwa hilo Neno. Kwa kweli litafanya hivyo. Unaona? Litafanya hivyo. Litasababisha mhemuko. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Pentekoste. Iliishia chini ya mhemuko. Ndivyo ilivyokuwa kwa kitu hicho chote!

191 Uinjilisti, ni jarife linalotupwa. Yesu alisema, "Linalotupwa baharini." Na wakati alipolivuta, lilileta kasa, kasa wa maji baridi, nyoka, vyura, na cho chote kile ndani yake. Bali kumbuka, hivyo ndivyo walivyokuwa tangu mwanzo. Kulikuwa na samaki mle, pia. Kazi yetu sisi ni kuvua. Ni kazi ya Mungu kusema ni nani samaki na ni nani siye. Unaona? Kwa nini wasifanye hivyo? Kama wangaliingizwa ndani kabisa katika Ufalme wa Mungu, hao elfu thelathini, kama yule mmoja wa Paulo alivyoingizwa, wakati aliporudi angepata mia nne na thelathini elfu. Unaona? Kwa maana mioyo yao ingekuwa inawaka moto.

192 Kama vile maskini Ndugu Crow alivyosema jana usiku. Nilipenda ujasiri wa—wa—wake. Nilipenda msimamo wake, kushikilia imani yake. Wakati Nuru inapoangaza, huyo hapo amesimama. Kamwe hutaweza kumtupa katika mojawapo ya mifumo hii, kama akikaa jinsi alivyo, na halafu kuendelea namna hiyo. Jinsi ninavyompenda mtu wa namna hiyo! Ndio, bwana.

193 Hebu mtu ye yote aseme kama ninafanana na kishale cha hali ya hewa. Afadhali nifanane na kishale cha hali ya hewa, kwa ajili ya Mungu, kuliko mtu aliyejipaka majivu Jumanne ya

Majivu kwa ajili ya Ibilisi. Huna budi kufanana na kitu fulani, hata hivyo. Hiyo ni kweli kabisa. Haya basi. Lakini, unaona, mambo ya mifumo ndiyo tunayoyaishi na kuyatendea kazi leo. Haya basi. Jambo lote limeoza, hadi kwenye kiini.

194 Sasa tuna akina ricky wetu kule. Sasa mtafanya nini naye? Unaona? Wanaingia tu kasi kama—kama kunguru. Kweli kabisa. Baraza lote la mawaziri, kitu hicho chote, kila kitu, mfumo wa mamilioni ya dola. Hivyo ndivyo mnavyotaka. Hivyo ndivyo kanisa linavyotaka. Hiyo ndiyo sababu mliingia. Ni rahisi sana sasa kuingia makanisani. Loo, jamani! Wapentekoste, yote yanayokupasa kufanya ni kutetemeka kidogo, kuruka-ruka kidogo, ama useme una ushuhuda fulani. Kila mtu anaweza kushuhudia.

195 Mnapaswa kwenda na mimi huko India, siku moja, na mwasikilize hao Wahindu wakishuhudia. Wangekufanya ujionee aibu, wewe mwenyewe. Hakika. Mnapaswa kwenda huko ndani ndani Afrika, hao Wahotentoti, basi acha waue mnyama na kujipaka damu mwili mzima. Sikiliza shuhuda zao, na mihemuko yao, na kunena kwa lugha, hakika; wakiabudu sanamu, iliyonyunyiziwa damu.

196 Ee Mungu, laiti ningaliweza kumfanya kila mtu hapa kuona jambo hilo! Hakika. Ibilisi huiga kila—kila kitu Mungu anachotoa. Yeye anakiiga. Hata na kweli ya Mungu, yeye huiga. Hiyo ni kweli kabisa. Angalia. Hao hapo. Lakini kanisa linataka nini?

197 Taifa linataka kitu fulani linachoweza kupata, si rais fulani kule juu, angeketi kitako kule katika baraza la mawaziri, angekomesha upuuzi huu, na kuondosha kabisa katika miji hii kwa . . . wauza pombe, inabidi wajiandae nusu saa wapate unyevu wa kutosha kutema mate. Lakini—lakini ha—hawataki kitu kama hicho. Wanataka jamaa fulani kitini atakayewapa pombe yote wanayotaka, na kuihalalisha, kisha wamtie mbaroni akilewa kupita kiasi; na—na kubaka, na hospitali za wenda wazimu, na cho chote kile, na maelfu ya ajali za barabarani, madereva walevi. Nao wanatoka wanaenda hapa barabarani, na mnamwachia dereva mlevi atoke aende huko na kumkanyaga mtu fulani na kumwua, ati yeye anasamehewa. Na, kwangu mimi, ni mauaji ya kudhamiria.

198 Hebu jamaa fulani atoke, akisherehekea, na atoke nje na afyatue bastola, mara mbili ama tatu, hewani, nao watamfunga huko ndani kabisa korokoroni hata ataoza kabla hujamtoa. Ni kitu gani? Haya basi. Hiyo hapo mifumo yenu ya ulimwengu. Hakuna haki ndani yake.

199 Mtu huyu, akizungumza juu ya serikali ya Marekani. Hakika, kila serikali duniani inatawaliwa na Ibilisi, kila mfumo. Kila . . . Yesu alisema hivyo. Shetani alikiri, "Hizi zote ni zangu.

Ninafanya nazo jinsi nipendavyo." Tuko wapi, sasa, siku hizi? Angalia mahali tunaposimama.

Sasa nisemeje, katika kufunga haya, ewe rafiki?

200 Mnaona ulimwengu wa kisiasa unaporomoka. Tunarudi moja kwa moja Rumi, hapa katika Marekani, mbio sana tuwezavyo kwenda. Biblia ilisema tungefanya hivyo, Ufunuo 13. Nasi tuko hapo. Ilifanya nini? Ilibidi wawe na kundi kubwa la madhehebu, fungua katika Ufunuo 17, "Mama kahaba wa kale na binti zake wote." Huyo hapo anarudi moja kwa moja, akiwa pamoja na kila madhehebu. Ndivyo mambo yalivyo. Wana Farao aliyeinuka, asiyemjua Yusufu, nasi hapa tunakwenda, kitu hicho chote. Na hata viongozi wetu wa Kipentekoste, wakiongoza kila mtu moja kwa moja kwenye ubembe huo mkubwa wa Hollywood, na kuwateka watu, kwa mmezo mkuu. Kwa ninii . . . Loo, ni ninii . . .

Mungu, lisaidie taifa hili. Mungu, wasaidie watu hawa.

201 Mara nyingine ingemfanya mtu kujisikia kama kuingia mitaani na kupiga mayowe. Bali ninajua Biblia inasema, ya kwamba, "Hakuna mtu anayeweza kuja asipovutwa na Baba Yangu." Ninajua ya kwamba mambo haya hayana budi kuwa yakitukia katika siku hizi. Ninaona hiyo Nuru, Nuru ya Mungu, ikienea. Ninaona walio wa uongo huko nje; na kumeka kote na . . . ama, urembo na kumeka, pamoja. Basi yanibidi kufanya nini?

202 Bwana Yesu, nisaidie niwe mwaminifu mpaka utakapokuja. Jalia nisimame, Ee Mungu. Jalia nichukue msimamamo wangu na kukaa hapa, Bwana, nipige hatua jinsi unavyopiga Wewe.

203 Ninaweza kuwaambia nini watu wale wanaomwamini Mungu kweli kweli? Nilisimulia mambo ya kutisha. Nina kama kurasa ishirini hapa, lakini nimeisha chelewa sana, juu ya muhtasari mfupi nilioandika kwa ajili ya somo. Inanipasa kusema nini asubuhi ya leo? Niwaachie nini? Ama, mko wapi?

204 Nimekemea madhehebu yenu, si kuwakemea ninyi. Ninaulaumu mfumo ambao umewafikisha mahali mlipo. Siwakemei ninyi, ndugu zangu wahudumu. Mnanichukua vibaya. Ninajaribu kuwasaidia. Vipi kama ningewaona kwenye boti mkielekea kwenye mkondo wa mto, kuelekea kwenye maporomoko, nami nilijua boti hiyo haiwezi kupita kwenye maporomoko hayo? Nami ninawapigia makelele, "Tokeni humo!" Si kwamba siwapendi. Ni kwa sababu ninawapenda. Mfumo huo mlio nao utaenda kuzimu ambako ulitoka.

205 Nilikuwa nikizungumza na mzee fulani hivi majuzi. Mvulana mdogo alikuja dukani, kule Tucson ambako nilikuwa. Akaingia kwenda kununua K Maalum cha—chache kwa ajili ya kiamshakinywa. Kulikuwa na mvulana mdogo amesimama pale, akinunua sigara. Kasema, "Hizi ni za nani, mama yako?"

Akasema, "La. Ni za yule mvulana anayeketi pale."

Kasema, "Yeye ana umri wa kutosha?"

Akasema, "Ndiyo."

206 Nikamwambia huyo mtu mwenye duka, nikasema, "Hatakuwa na umri wa kutosha kamwe." Unaona? Lakini unaninii . . .

207 Wa—watu wanaanza kufikiri ya kwamba hilo ni sawa. Kuvuta sigara ni sifa. Na makanisa yanajizoeza tu kunywa pombe kiasi, kunywa pombe tu kwa kisasa. Loo, jamani! Unaninii . . . Umetoa kitu hicho wapi? Kimetoka katika mfumo fulani, si kutoka kwenye Neno la Mungu. "Yeye anayempa jirani yake pombe kali." Unaona? Hakika, ndivyo ilivyo. Ni—ni maangamizi, ufisadi wa taifa letu, ubembe wa Hollywood. Na hapo ndipo tumefikia, katika machafuko kama hayo. Sisi hapa katika hali ya namna hiyo.

208 Mzee huyu akaniambia, akasema, "Vema," akasema, "Ninamsikitikia." Akasema, "Kwa namna fulani ni vigumu kutoka—kutoka . . . kwa jambo hilo, kwetu sisi kuacha. Ni vigumu? Si ingekuwa ni vigumu kwako kuacha?"

Ni kasema, "Sijawahi kuanza."

209 Akasema, "Loo, kumbe huvuti sigara." Akasema, "Ninakusifu, rafiki yangu." Alikuwa ana umri wa kama miaka sabini.

Nikasema, "Asante."

Akasema, "Kama vile wiske, ni vivyo hivyo."

Nami nikasema, "Sinywi pombe."

210 Akasema, "Vema, napenda hilo." Akasema, "Ninafikiri ni ninii . . . Kama mtu anataka kuja nyumbani, anywe gilasi ya pombe," akasema, "ni sawa. Lakini wakati wanapowachukua hawa wanawake, nao wako huko mitaani, na wanafanya yasiyofaa, wamelewa, na kuzurura . . . Mumewe anaenda kazini, halafu wanachukua gari, na kutoka wanaenda zao."

211 Nikasema, "Hawapaswi kamwe kumruhusu mwanamke kuendesha gari." Jamani, kama ningalikuwa kule, asingeliendesha gari, kama ningalikuwa na jambo lo lote la kusema juu ya jambo hilo.

212 Wao husema wanawake ndio madereva wazuri kuliko wote. Mimi ni msafiri wa kimataifa. Mimi na mwanangu, wakati tunapita katika nchi hii, tunaweka kitabu kwenye ga—gari. Na kila wakati mtu alipopatikana na hatia ya barabarani, akaelekezwa kando ya barabara, tuliweka alama "mwanamume" ama "mwanamke." Na kati ya visa mia tatu, vilivyosababishwa na wanawake vilikuwa ni mia mbili themanini na moja; kumi na tisa vilisababishwa na wanaume. Hiyo ni kweli kabisa. Hata hivyo, ataketi hapo na kupandisha

nywele zake juu. Na atageuka namna *hii*, na kujipendekeza, na kila kitu. Lakini, loo, hapana shaka, polisi hawatamripoti. Wanao kwenye kikosi cha polisi. Ni fedheha jinsi gani!

213 Mwanamke anapotoka nyuma ya meza jikoni, nyumbani, akishughulikia maskini huduma yake mwenyewe aliyopewa na Mungu, watoto wake wachanga, yeye yuko nje ya mapenzi ya Mungu.

214 Hebu umweke mimbarani, yuko nje ya mapenzi ya Mungu. Hakuna Andiko kwa mwanamke mhubiri. Ninataka mwanamume fulani asimame na anipe hilo, anitazame usoni. Hakuna kitu kama hicho. Jambo hilo, Pentekoste ndio chanzo cha upuuzi huo. Haijawahi kuwa hivyo! Adamu aliumbwa kwanza, halafu Hawa. Adamu hakudanganywa. Lakini, hata hivyo, mnafanya jambo hilo. Sasa mnaona mahali ambapo mmejipeleka? Mmejitenga mbali sana huku, hivi kwamba, hamwezi sasa kurudi tena. Bali mnaenda zenu tu. Naam. Huo ni ulimwengu. Hivyo ndivyo mnavyotaka. Hivyo ndivyo mnavyotaka. Hicho ndicho mlicho nacho. Unaona?

215 Lakini kwa wale wanaoutazamia Ufalme Ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu, sisi tunaupokea Ufalme.

216 Hatutafuti madhehebu. Hatutafuti. . .Ingawaje, wale wanaompenda Mungu, hatutafuti mtu mwenye kipaji cha kimadhehebu. Hatumtafuti mwanahisabati fulani mkuu anayeweza kusimama hapa juu na kutwambia jinsi ya kuanzisha hisabati mpya, na kadhalika, na kutoka kwenda mitaani na kujichosha nusura kufa kuleta wafuasi. Mna nini? Mnaleta nguruwe zaidi kwenye zizi. Hivyo tu. Nao wanapata nini wanapofika pale? Kinyaa. Kweli kabisa.

Mungu huwazaa katika Ufalme, huko Juu. Hiyo ni kweli kabisa.

217 Mvulana fulani alikuwa anamkemea Billy Graham, nadhani mlisoma hilo kwenye gazeti la *Post*, juu ya yale aliyokuwa amefanya. Bob Jones alisema Billy Graham. . .Bob Jones hupiga makelele sana, sivyo? Kweli. Billy Graham amefanya mengi zaidi kwa ajili ya Ufalme wa Mungu katika miaka hii michache amekuwa hudumani, kuliko Bob Jones angalifanya kama alingalikaa hapa kwa muda wa miaka milioni moja zaidi. Hiyo ni kweli. Lakini yeye anasema nini? "Billy Graham anatoka tu na kusema, vema, yeye hana madhehebu, anawapeleka kwa hayo." Mungu ambariki mtu huyo kwa jambo hilo. Naam, bwana. Mnafanya nini? Mnamleta, mnamfanya mwana wa kuzimu maradufu, kuliko alivyokuwa, mlipomchukua huko mtaani.

218 Wanafunzi kamwe hawakuwapeleka kwenye madhehebu yo yote. Waliwafanya wajazwe na Roho Mtakatifu na kuingia katika Ufalme wa Mungu. Na hapo Roho Mtakatifu anachukua mamlaka. Naam, bwana.

219 Sasa, lakini walisema aliwiwa na kanisa, kwa kutojiunga na ma madhehe-. . . kuwaachilia wote waingie kwenye madhehebu. Nadhani wote wanapaswa kuwa wafuasi wa Chuo cha Bob Jones. Unaona? Basi kweli walikuwa wametoka mahali pao. Sasa, na hawa wote hapa wanaoitwa, wakereketwa wa kimsingi, na upuuzi wote huu hapa. Ni upuuzi.

220 Tunatafuta nini, enyi marafiki? Sisi ni akina nani? Kanisa halisi halitafuti madhehebu fulani, halitafuti rais, halitafuti mtu mwenye kipaji ainuke. Bali linautafuta Ufalme na Mfalme anayekuja. Ufalme ni nini? Umo duniani sasa. Ni Roho, Mwili wa kisiri wa Kristo. Katika huo, wametoka kwenye Presbiteri, Wamethodisti, Wapentekoste, na kila kitu. Wako katika Ufalme huu. Wamezaliwa ndani humo. Wanaingia Mle kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, nao wamo kwenye Ufalme huu. Nasi tunamtazamia Mfalme kuja kwenye Ufalme huu, ambaye ataanzisha Ufalme Wake hapa duniani, kwenye ninii Chake— kwenye kiti Chake cha enzi, kiti cha enzi cha Daudi. Atatawala na kumiliki milele. Hilo ndilo Kanisa linalotazamia.

221 Na jambo zuri kuhusu hilo, enyi marafiki, ni, wazieni jambo hili. Kabla hatujafika kwenye Ufalme huu. . . Kabla Ufalme huu haujaja, sasa tunaweza kuketi pamoja katika Ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tumeinulia juu ya vivuli vyote vya upotovu wote wa ulimwengu, na vipindi vyao vyote vya televisheni, na upuzi huu mwingine wote walio nao duniani leo, na upotovu wao wote uliooza na mifumo, na kila kitu. Tuinuliwe juu katika Ulimwengu wa Roho! Naye Roho Mtakatifu, Mwenyewe, aje juu yetu, na kuzungumza na kutuambia dhambi zetu, na kutwambia jinsi ya kujiweka sawa, na yale tuliyofanya maishani, na yale tunayofanya. Ni Roho Mtakatifu, Yesu Kristo Yeye yule jana, leo na hata milele. Huyo ndiye Mfalme atakayekuja kwenye Ufalme Wake siku moja. Na Ufalme Wake sasa unaimarishwa katika mioyo ya watu Wake hapa duniani.

222 Mungu awabariki. Kama sitawahi. . . Huenda msinipende baada ya haya. Unaona? Huenda msinipende, lakini siku moja mtatambua ya kwamba Hiyo ni Kweli. Sasa, Mungu awabariki. Sitawaweka kwa muda mrefu zaidi, bali ninataka mkumbuke jambo hili.

223 Tunautarajia Ufalme, nasi sasa tunaupokea Ufalme ambao hauwezi kutikiswa. Tunapokea kitu fulani mioyoni mwetu, kwamba hakuna pepo jehanamu wanaoweza kuukitikisa. Hakuna cho chote.

224 Mzee huyu pale, hivi majuzi, alisema, "Vema," alisema, "hebu nikwambie." Akasema, "Jambo lenyewe ni hivi, bwana." Nilimwambia nilikuwa mhudumu, ndio sababu sikuvuta sigara wala kunywa pombe, na kadhalika. Akasema, "Vema, ni— ninapenda jambo hilo." Akasema, "Hiyo ni kweli." Akasema,

"Nilipokuwa kwenye jeshi la polisi, kila kitu," akasema, "ilikuwa ni uhalifu wa vijana. Huo tu ndio tulio nao siku hizi."

225 Nikasema, "Bwana, sitaki kutokubaliana nawe. Lakini," nikasema, "si uhalifu wa vijana. Ni uhalifu wa wazazi. Wazazi ndio wahalifu, hiyo ni kweli, wanapowaachilia watoto wao kutenda jinsi hiyo." Wanahitaji ninii . . .

226 Hapo, ninyi, mlifanya nini? Mliweka gazeti la *Hadithi ya Kweli* mezani penu, badala ya Biblia. Badala ya mikutano ya maombi, iliwabidi kukimbia mahali fulani na kufanya jambo jingine. Hiyo ndiyo shida ya ulimwengu siku hizi. Hiyo ndiyo shida ya watu wetu wanaoitwa Wakristo; kucheza dansi, karamu, na urafiki wa kunywa pombe, na, loo, kila kitu. Unaona? Ni uhalifu wa wazazi, si uhalifu wa watoto. Mzazi ndiye mhalifu. Ni yeye. Angalia.

227 Nikasema, "Ilikuwaje, bwana?" Nikasema, "Wewe unayesimama hapa. Sisi ni wanaume wawili ambao hatujawahi kukutana hapo nyuma, maishani. Wewe ni ninii . . . " Alisema alikuwa na umri wa miaka sabini na kitu, akifanya tu jambo hilo pembeni. Nikasema, "Mimi ni mhudumu." Kisha nikasema, "Unawakilisha sheria za nchi. Ninawakilisha sheria za maadili ya nchi." Ndipo nikasema, "Sasa, kama mtu fulani alivunja sheria zenu za nchi, nini kilitukia? Mliwafunga gerezani, sivyo? Mliwapeleka moja kwa moja gerezani kama walivunja sheria zenu za nchi."

Akasema, "Hiyo ni kweli."

228 Nikasema, "Kama wakivunja sheria hizi wanaenda kuzimu." Nikasema, "Hakimu mwenye haki ambaye . . . Mungu, kwa Neno Lake . . . Kesi hizo zinaamriwa kulingana na sheria za taifa. Na zikipatikana kwamba zimevunjwa, basi hakuna kitu ila kuadhibiwa. Na sheria yo yote isiyokuwa na adhabu si sheria. Kweli." Nikasema, "Kuvunja sheria ya Mungu, Neno Lake, ni utengano wa Milele kutoka katika Uwepo Wake." Nikasema, "Sasa unaona mahali tulipo."

Akasema, "Bwana akubariki. Je! unahubiri wapi?"

Basi nikasema, "Mahali po pote tu ninapoweza kupata mlango wazi."

229 Haya basi. Unaona? Mzee tu mwenye umri huo, unaona, naye akiliona tu hilo wakati huo. Kuvunja sheria za Mungu, ambazo ni Neno Lake, nawe unaelekea jehanamu. Ni hilo tu. Mtumikie Mungu sasa.

230 Tunaingia katika Ufalme huu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na wakati tunapoingia Mle, si kujifanya tunaamini. Wengine, mimi si- . . .

231 Sasa, wewe, usi—usiweke jambo hili niani mwako, "Sasa, Ndugu Branham haamini ya kwamba unanena kwa lugha."

232 Ninaamini mnanena kwa lugha. Lakini waangalie tu hao wanaonena kwa lugha, wala hawajampata. Angalia ninii... Angalia jinsi wanavyoenenda na jinsi wanavyotenda. Unaweza kujua hawajampata. Unaona?

233 Angalia makanisa siku hizi, yanasema, "Sisi ndio Kanisa." Kila mmoja wao, "Sisi ndio Kanisa."

234 Kuna Kanisa moja tu, na hilo ni mwili wa kisiri wa Kristo. Unapoingia Mle, unabatizwa Mle kwa Roho Mtakatifu, na jambo Hilo linabadilisha utu wako wote.

235 Si muda mrefu uliopita. Nitasema jambo hili, kuhusu tu jambo fulani lililoingia moyoni mwangu. Mimi na mke wangu, kwenye msimu uliopita wa kiangazi, nilikuja nyumbani, kutoka kwenye mmoja wa mikutano. Tulienda kununua vitu dukani. Tukamwona mwa—mwanamke aliyekuwa amevaa sketi. Lilikuwa ni jambo geni nchini mwetu. Wote wako uchi. Kwa hiyo, basi, tulimwona mwanamke huyo. Yeye...Nasi tuliwatambua baadhi ya wanawake hao kwa—kwamba wao ni wafuasi na wanaimba kwenye kwaya huko makanisani. Naye akasema, mke wangu akasema, "Billy, ni kitu gani kinachowafanya hao wanawake..." Kasema, "Kwa nini—kwa nini wanafanya hivyo?" Kasema, "Watu wetu..." Kasema, "Nashangaa ni kwa nini?"

236 Nikasema, "Si—si—sisi hatuko hivyo. Sisi si wa ufalme huo." Naye akasema... "Vema," nikasema, "hao sio watu wa aina yetu."

237 Naye akasema, "Una maana gani?" Kasema, "Hivi sisi si Wamarekani?"

238 Nikasema, "Loo, la. La, bwana." Nikasema, "Ninaenda huko Ujerumani, ninakutana na roho ya Kijerumani, roho ya taifa. Ninaenda Sweden, ninakutana na roho ya Kiswideni. Ninaenda India, ninakutana na roho ya kitaifa. Unakuja Marekani, unakutana na ricky, roho ya namna hiyo, loo, mjuvi."

239 Waangalie wanapokuja kwenye nchi nyingine. Inakuchefua hata kukufanya ufikiri kwamba wewe ni Mmarekani, jinsi vile wanavyofanya. Hiyo ni kweli. Ndio watu wenye matendo machafu kuliko wote, wenye jeuri kuliko wote, majuha huru, wenye elimu. Hiyo ni kweli. Na walimwengu wengine wanajua hivyo. Si ajabu, tunajaribu kununua urafiki wetu kwa dola zetu. Hununui urafiki. Sasa, kuna njia...Taifa letu limeoza mpaka kwenye mizizi. Hiyo ni kweli. Hakuna tumaini kwake. Lote limekwisha. Kuna jambo moja tu la kutazamia, kule Kuja kwa Bwana. Naam.

Akasema, "Vema, hivi sisi si Wamarekani?"

240 Nikasema, "La. Tunaishi hapa. Tunaishi hapa. Hakuna..." Nikasema, "Vema," nikasema, "unaona, watu hao ni Wamarekani. Wana Roho ya Kimarekani. Wanatenda kama

Hollywood, ambayo inaitawala Marekani: vaa yake, mitindo yake, mungu mke wake, na kadhalika. Hivyo ndivyo wanavyofanya kabisa. Sasa," Nikasema, "Hao ni Wamarekani. Sisi tumetoka Juu. Hao wanawake kanisani mwetu, hawafanyi hivyo. Wanaishi maisha matakatifu, wasafi."

241 Hebu mchukue mwanamke anayevaa nguo za namna hiyo, na anatoka anaenda mtaani. Sijali jinsi unavyojaribu kuishi kiadilifu, kwenye mwisho wa wakati, utaitwa mzinzi. Kama mwanamume ye yote akikuangalia, akutamani, nawe ndiwe uliyejianika mbele zake, una hatia ya kufanya uzinzi. Yesu alisema hivyo. Huenda ukawa msafi sana kwa mumeo ama mvulana mpenzi wako, kama uwezavyo kuwa. Lakini kama ukivalia namna hiyo na mwenye dhambi fulani anakuangalia, itambidi kuwajibika kwa hilo, kwenye ile Siku ya Hukumu, nawe ndiwe uliyejianika.

242 Jisafisheni, enyi wanawake. Mrudieni Mungu. Hiyo ni . . . Sijali wanayosema juu yako. Mrudieni Mungu.

243 Wanawake walikuwa wakiheshimiwa sana. Yeye ndiye uti wa mgongo wa taifa. Na sasa yuko wapi? Yeye amejiletea hayo. Anadhaniwa . . . Hata watu hawavui kofia zao, wanapoongea nao, wala cho chote kile. Ni hali hiyo tu. Wangefanya nini? Wamejiletea jambo hilo.

244 Kwa nini lilianza? Ricky fulani nyuma ya mimbara, mwenye namna fulani ya ujuzi wa seminari, kibaraka wa madhehebu fulani, badala ya mtu wa Mungu kulichukua hilo Neno na kuwararua vipande-vipande Kwalo. Kweli. Hao ndio tulio nao kanisani.

245 Mungu, turehemu. Jalia twende kwenye Ufalme huu. Hebu na twende ambako tunaweza kupata na kuishi kulingana na Ufalme huo, ndipo mawazo ya—yako ni matakatifu. Mambo yako, mawazo yetu, yako huko Juu, ambako urithi wako unadumu.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

246 Kwa uchaji, ninawauliza swali hili. Baadhi yenu huenda hata msirudi usiku wa leo. Huu unaweza kuwa ndio wakati wangu wa mwisho wa kuwaona duniani. Yesu anaweza kuja kabla ya usiku. Maangamizi yanaweza kutokea kabla ya usiku. Kunaweza kukatukia, unajua, wakati wo wote, Kule kuja kwa siri kwa Kanisa.

247 Unasema, "Ndugu Branham, kitambo kidogo kilichopita, wakati uliposema, 'Kanisa lingeweza kwenda wala tusingejua'?" Loo, ndio. Biblia inasema hivyo. La, hawatajua kitu juu ya jambo hilo. Ni Kuja kwa siri. Yeye anakuja kwa siri na kulichukua Kanisa Lake kisiri. Analichukua, kama kitabu kimoja nilichosoma wakati mmoja, cha Romeo na Juliet. Unaona? Yeye anakuja kumchukua, hakuna mtu ana habari.

248 Ulimwengu utasema, vema, wawili ama watatu kutoka kwa hawa, watasema, “Vema, mtu fulani alipotea jana usiku.” Na huko mbali nchini, wawili ama watatu zaidi. Hivyo ndivyo Yeye alivyosema ingetukia. “Loo, walitoka wakaenda mahali fulani. Wao. . . Msichana fulani alifanya kosa. Alitoroka. Mwanamume fulani, alitoroka, mke wa mtu mwingine.” Wamenyakuliwa. Wala hawajui kitu juu yake. Mamia yao wanaenda kila siku, wala hawajui kitu juu yake. Unaona?

249 Kabla wakati huo kuja, mbona usijiweke sawa na Mungu? Sina budi kukutana nanyi kwenye ile Hukumu. Ninawapenda. Siwakemei Wapentekoste kwa sababu. . . Siji kamwe miongini mwenu nipate kufadhiliwa nanyi. Mimi ninakuja kwa sababu Mungu alinituma. Ninakuja katika Jina la Bwana Yesu. Je! nimepata kuwaambia jambo lo lote lisilo kweli? Je! mmoja wa viongozi wenu amewahi kusimama na kuniambia nilikuwa nimekosea? Ningewaomba wathibitishe jambo hilo. Wanajua vizuri zaidi ya hivyo. Vema. Sasa, mmeninii. . . Wengi wenu wamekuwa mikutanoni. Nanyi mnajua ya kwamba nisingesema jambo hili, asubuhi ya leo, isipokuwa nimejua ya kwamba jiji hili linalihitaji. Limetumbukia kabisa katika kila uchafu na kinyaa. Mnamhitaji Kristo.

250 Je! mngetaka kupokea Ufalme halisi wa Mungu, ambapo utu wako wote unabadilishwa; unabadilishwa na unafanywa kiumbe kipya; kuchanua kabisa kwa Maisha, kwa Uzima wa Milele, umo ndani yako; je! mambo ya dunia yamekufa? Sitawaomba mje kwenye madhabahu yo yote. Nitaomba kwa uaminifu wako. Kama kweli una shauku, na unataka mimi niombe, ninapofunga ibada, inua mkono wako, useme, “Niombee, Ndugu Branham.” Mungu akubariki. Vyema, yapata kama asilimia tisini.

251 Baba yetu wa Mbinguni, nilipoangalia hapa chini kabla sijafunga macho yangu, Bwana, na kuona gazeti hili hapa, tangazo hili kwenye gazeti, “hadithi ya Tony Fontane,” wanawake wenye nywele za shaba, vitimbi, wakicheza dansi jukwaani, muziki, wamevalia kizinifu, na wanaume.

252 Yesu alisema, “Mlitoka mkaenda kuona nini wakati mlipoenda kumwona Yohana; mtu mwenye mavazi mororo, ukosi uliopinduliwa, na kadhalika? La.” Kasema, “Wako kwenye majumba ya wafalme. Mlienda kuona u—unyasi unaotikiswa na upepo; mtu ye yote ambaye angetaka madhehebu yanayotoa kitu kidogo kilicho bora kidogo kuliko hayo mengine, na angeyaendea? Si Yohana. Yeye hakuwa unyasi unaotikiswa na upepo. Yeye kamwe hakupatana juu ya mambo yenu yo yote.” Kasema, “Mlienda kuona nini, basi, nabii?” Kasema, “Ninawaambia, zaidi ya nabii.”

253 Baba yetu, Mungu, tunatambua ya kwamba hakuna matumaini yaliyosalia kwa ajili ya madhehebu ya kanisa.

Yamekwisha, Bwana. Yalikuwa ni kinyume cha mapenzi Yako, hapo mwanzo. Hakuna matumaini kwa taifa hili. Limekwisha.

254 Tumeona, taifa hili, ni mfano mkamilifu wa Israeli. Jinsi ambavyo wakati Israeli walipokuja kwenye nchi ya uenyeji wao, na—na wakawafukuza wenyeji, kama vile tulivyokuja na kumfukuza Mhindi wa Kimarekani. Na jinsi wao walivyokuwa na watu mashuhuri katika siku hizo: Daudi, Sulemani, Yoshua. Na vivyo hivyo nasi tulikuja na kuwafukuza wenyeji, na kuimarisha nchi yetu, uchumi wetu, juu ya uhuru wa kuabudu, wakati tulikuwa tumefungwa na mafundisho ya sharti na kadhalika. Tulikuwa na watu mashuhuri, akina Washington, Lincoln. Lakini, hatimaye, miaka iliposonga mbele, wao hatimaye walimchagua Ahabu aliyekuwa na Yezebeli aliyejipaka rangi ambaye aliweka mitindo ya ulimwengu. Vivyo hivyo tumefanya jambo lile lile kabisa. Na sasa tunaona jambo lile lile likitukia. Katika siku hiyo, ulikuwa na Eliya aliyesimama na kukemea jambo hilo. Loo, jinsi walivyomchukia, bali yeye—yeye alisimama. Sauti yake ingali itakuwa imesimama kwenye ile Siku ya Hukumu.

255 Na, Baba, tutumie Eliya fulani. Tutumie Sauti ya Biblia, Sauti ya Mungu, na uithibitishe. Na uthibitishe ya kwamba Wewe ni Mungu, ya kwamba unafanya vile vile jana, leo, na hata milele, kwamba watu wapate kujua. Bila wasiwasi wo wote, wanaona ya kwamba ni Kweli. Na jalia watu . . .

256 Kama vile maskini yule mwanamke kisimani, alikuwa amechanganyikana na upuuzi wa kila namna, lakini wakati Nuru ile ilipoangazia maskini njia yake aliyokuwa anapitia, aliona jambo fulani. Hakuwa tena jinsi alivyokuwa tangu wakati huo. Alikuja kwenye Chemchemi ambayo hakuwa ametembelea hapo awali.

257 Tujalie, Bwana, leo, ya kwamba wengi leo wataona ya kwamba kuna Kisima kilichofunguliwa, na Neno la Mungu lingali linatenda kazi kwa kila mtu ambaye ataamini na kulipokea. Mikono mingi iliinuliwa, Bwana Yesu. Wao ni wahitaji sana. Ninaamini wao wanamaanisha jambo hilo. Ni vigumu kwangu kufikiri ya kwamba—kwamba watu wanaojaribu, na wameingia kwenye shirika hili la Kipentekoste, kwa sababu kwamba wametoka kwenye mitindo hii na kadhalika, na kuona haikuwafaa kitu. Nao wamekuja papa hapa, wakajikuta katika kundi hili la—la Hollywood, aina ile ile ya utaratibu wa elimu, watu mashuhuri, kama tunavyowaita hapa duniani, Bwana. Loo, jinsi . . . Mungu, wasaidie. Sivyo, Bwana?

258 Nami nina—ninaamini ya kwamba wasingeweza kuinua mikono yao, pasipokuwapo na kitu Fulani pale kuwafanya wainue mikono yao. Kuna Roho fulani anayewazunguka. Na wanaume hawa na wanawake, asilimia tisini yao, labda, Bwana,

kwamba wanatambua ya kwamba kuna kasoro fulani, nao—nao hawataki iwe hivyo. Na sasa, kulingana na sayansi, wasingeweza kuinua mkono huo; nguvu za uvutano zinashikilia mkono huo chini. Lakini wanaweza kuiasi sayansi, kwa maana wao ni wanadamu na wana roho ambayo inaweza kuamuru mkono huo uinuliwe, na utainuliwa.

259 Na, Mungu, Uliwajalia sana wanadamu. . .kwa uhuru wa kuchagua, kutoa maamuzi yake mwenyewe. Na sasa kuna roho fulani inayosimama karibu nao inayowaambia ya kwamba roho ile ile waliyokuwa wakiiabudu wakati wote imekuwa inadanganya, nao wanataka uamuzi. Na Roho inayowazunguka, Roho Mtakatifu, inawafanya wainue mikono yao na kusema, "Nipe Mungu." Bwana, unajua mioyo yao. Ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atakuja aingie kwa nguvu, kama bwawa linalovuja mahali fulani, na akiba ya matarajio yaendayo kasi ya Roho Mtakatifu yatahuisha nafsi zao kwa Moto halisi, wa upendo wa Mungu unaowaka kule, kwa ajili ya wanadamu wanaokufa; si kwa ajili ya madhehebu, bali kwa ajili ya wanadamu wanaokufa, si kwa ajili ya siasa, wanapoona ulimwengu wa kimadhehebu ukiporomoka. Wanaona ulimwengu wa kisiasa ukiporomoka. Na ninii. . . Umoja wao wa Mataifa, puto kubwa mno la mpira ambalo linasukumwa kila upande na kila upepo wa—wa sera za kisiasa, linasukumwa huku na kule. Na, Ee Mungu, wanaona ninii. . .baraza hili la makanisa, kama wanavyoliita. Wanaona linawapeleka moja kwa moja kwenye mtego, Bwana, kama buibui akifuma utando.

260 Mungu, jalia Pentekoste iamke, upesi, Bwana, ukiwa ni wakati wanapoweza kuamka. Amsha jiji hili dogo hapa, Bwana. Waamshe wanawake hawa wanaoketi hapa. Waamshe wanaume hawa. Usiache lipite, Bwana.

261 Kama vile kanisa la Katoliki, lilivyoamka baada ya Mtakatifu Patrick. Kama kanisa la Kiyahudi, lilivyoamka baada ya Eliya, kisha wakalipamba kaburi lake. Kama vile kanisa Katoliki, lilivyoamka baada ya Joan wa Arc. Hawajui jambo hilo wakati linapoendelea. Lakini likiisha kupita, ndipo wanatambua. Kama vile kanisa, lilivyoamka baada ya Yesu kusulubishwa. Liliisha chelewa sana, wakati huo. Waliisha litenda jambo hilo tayari.

262 Ee Mungu, waamshe Wapentekoste. Ninawapenda, Bwana. Hao ndio watu. . .Wa—wanasaidia kuwalisha watoto wangu. Bwana Mungu, jalia wajue ya kwamba Ujumbe wa Mungu si lazima utoke kwenye kundi la madhehebu yao au mashirika yao. Wewe huinua unayetaka. Wewe ni Mungu. Zitikise nafsi zao asubuhi ya leo, Baba, na uwarudishe kwenye kutambua ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na sasa tunaketi katika Uwepo Wake, katika Ulimwengu wa Roho, tukiinuliwa juu na Neno. Hao ni Wako, Bwana. Fanya nao

jinsi unavyotaka. Ninawakabidhi Kwako, kama kumbukumbu la ushindi wa Ujumbe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

263 Ninampenda. Je! mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kama dada yetu angetupa tuni, "Nampenda. Nampenda." Je! mmenikasirikia? ["Hapana."] Kama umenikasirikia, njoo hapa unipe mkono, na tuombe. Unaona? Nimewaambia Ukweli, Ukweli unaouma, wa Injili. Siku moja huenda mkatambua jambo hilo. Usiache ukachelea sana. Twaweza kusimama, kwa muda mfupi tu?

Nampenda, . . .

Je! mnampenda? Inueni mikono yenu.

. . . Nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari.

264 Sasa, Wamethodisti peaneni mikono na Wabaptisti, wa umoja peaneni mikono na wa utatu, na kanisa la Mungu peaneni mikono na Waassemblies. Kila mmoja wetu, wakati tunapouimba huu, aseme kwa unyofu, "Ninakupenda, ndugu, dada. Nitakuombea. Wewe ni ndugu yangu, dada yangu." Hebu na tufanye hivyo tena sasa.

Nam-. . . [Ndugu Branham anazungumza na ndugu fulani—Mh.]
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mti-. . .

265 Sasa, Waasemblies of God, njoni mwangalie *Hili*, baadaye, kisha mtubu. Ombeeni madhebu yenu, au mtoke kwenye mfumo kama huo. Assembly of God lina baadhi ya watu halisi wa Mungu mle ndani. Ninawajua. La Umoja lina watu halisi wa Mungu miongoni mwao. Hiyo ni kweli. Kanisa la Mungu lina watu halisi wa Mungu. Baptisti, Methodisti, wana watu wa Mungu. Lakini hiyo mifumo ndiyo inayowafanya kuwa hivyo, vibaraka wa huo mfumo.

266 "Nam-. . ." Hebu tumwinulie mikono yetu sasa Yeye tunayempenda. "Nam-. . ." Na moyo wako wote sasa, "Nampenda."

Vema. Ndugu Demos.

*ULIMWENGU UNAPOROMOKA* SWA63-0412M
(The World Is Falling Apart)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa asubuhi, tarehe 12 Aprili, 1963, katika Western Skies Motel kule Albuquerque, New Mexico, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2007 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org